

Taarifa ya Mwaka ya Vodacom Tanzania Public
Limited Company

kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2020

Tunakuunganisha
kwa kesho
iliyo bora

Yajayo yanafurahisha,
Uko Tayari?

 **vodacom**

Taarifa ya Mwaka 2020 ya Vodacom Tanzania

Hii ni taarifa ya nne ya mwaka ya Vodacom Tanzania, na ya tatu tangu tuorodheshwe kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam tarehe 15 Agosti 2017.

Taarifa hii inatoa maelezo ya jumla ya biashara yetu, muundo wetu wa biashara, mazingira yetu ya uendeshaji, kupitia mikakati yetu ya uendeshaji na mfumo wa utawala kwa mwaka wa fedha ulioanzia tarehe 1 Aprili 2019 hadi 31 Machi 2020. Utaratibu wetu wa kutoa taarifa ya mwaka umekuwa ukiongozwa na kanuni na masharti yaliyo katika Viwango vya Kimataifa vya Taarifa za Fedha (IFRS), Kanuni za Soko la Hisa la Dar es Salaam za mwaka 2016 na Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002. Ernst & Young ('EY') amethibitisha taarifa zetu za fedha za mwaka na kutoa hati safi (kurasa 66 hadi 69).

Bodi imeshiriki kikamilifu katika uandaaji na uwasilishaji wa taarifa hii. Bodi inaamini kuwa ripoti hii inaelezea masuala yote muhimu na inawasilisha maelezo yenye ulinganifu kuhusu utendaji wa kundi la Makampuni kwa kipindi husika na vilevile inatoa taswira halisi ya mikakati yetu ya utekelezaji.

Wakurugenzi wanaamini kuwa kuchapisha mipango mkakati ya Vodacom Tanzania, hakutaleta athari yoyote ile katika medani za ushindani wa kibiashara. Bodi ilipitisha taarifa hii ya mwaka tarehe 14 Julai 2020.

Imesainiwa kwa niaba ya Bodi na

Mkatabungu

Margaret Ikongo
Mwenyekiti wa Muda

Hisham

Hisham Hendi
Mkurugenzi Mtendaji

Azma yetu ya kuongeza thamani katika jamii

Azma kuu ya Vodacom Tanzania ni 'kuunganisha jamii kwa kesho iliyo bora'. Malengo ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo Endelevu (UN SDGs) yanatoa taswira ya muonekano wa kesho iliyo bora, kwa kuweka malengo ya muda mrefu ya kuondoa umaskini, kulinda mazingira na kuleta mafanikio kwa wote ifikapo mwaka 2030. Vodacom Tanzania ina nia ya kutimiza wajibu kama taasisi ya sekta binafsi katika kufikia malengo haya, kuunga mkono serikali, jamii, biashara na watu binafsi kujenga kesho iliyo bora. Tunachangi kufikia malengo ya kitaifa na kimataifa ya maendeleo kupitia biashara yetu kuu kwa kuwezesha mawasiliano ya data, ujumbe, sauti na huduma za fedha.



Vodacom Tanzania imeainisha na kuweka kipaumbele katika malengo nane ya maendeleo endelevu ambayo tunaamini tunaweza kuwa na mchango chanya.



Yaliyomo

Maelezo ya jumla

1

| | |
|---------------------|---|
| Sisi ni nani | 1 |
| Thamani tuliyojenga | 2 |

Biashara yetu

4

| | |
|--------------------------------|---|
| Vodacom Tanzania kwa ufupi | 4 |
| Bidhaa na Huduma zetu | 5 |
| Taarifa ya Mwenyekiti wa Muda | 6 |
| Taarifa ya Mkurugenzi Mtendaji | 8 |

Utendaji wetu

11

| | |
|----------------------|----|
| Ufanisi wetu kifedha | 11 |
|----------------------|----|

Mfumo wa kiutawala

16

| | |
|-------------------------------|----|
| Viongozi wetu | 16 |
| Taarifa ya uongozi wa shirika | 18 |
| Taarifa ya masuala ya ujira | 24 |

Maelezo ya hesabu za fedha za mwaka

28

| | |
|------------------------------------|----|
| Taarifa ya wakurugenzi | 28 |
| Tamko la majukumu ya wakurugenzi | 35 |
| Tamko ka mkuu wa kitengo cha fedha | 35 |

Taarifa za ziada

36

| | |
|-------------------------|----|
| Taarifa ya Mkutano Mkuu | 36 |
| Fomu ya Mwakilishi | 41 |
| Taarifa kuhusu umiliki | 43 |
| Taarifa kuhusu Kampuni | 43 |
| Dai la Haki | 44 |

Maelezo ya msingi

Tafadhali zingatia kuwa hii ni tafsiri ya taarifa ya mwaka kwa ufupi. Taarifa kamili ya mwaka imetolewa kwa lugha ya kiingereza. Iwapo kutatokea mkanganyiko wa tafsiri, taarifa ya kiingereza itatumika.

Sisi ni nani

Vodacom Tanzania ni kampuni inayoongoza nchini Tanzania kwa kutoa huduma za mawasiliano kwa wateja wa matumizi binafsi na biashara ikiwa ni pamoja na huduma za simu sauti, data, ujumbe mfupi wa maneno, na huduma za fedha kwa wateja zaidi ya milioni 15.5.

Vodacom Tanzania iliorodheshwa kwenye soko la hisa la Dar es Salaam mnamo Agosti 15, 2017. Mmiliki mkubwa wa Vodacom Tanzania na kampuni zake tanzu (yaani 'Kundi la Kampuni za Vodacom') ni Vodacom Group Limited, kampuni iliyosajiliwa Afrika Kusini ambayo nayo inamilikiwa na Vodafone Group PLC ya Uingereza.

Kwanini tupo

Azma yetu

Kutoa huduma nafuu ya intaneti.

Tunakuunganisha kwakesho iliyo bora



Jamii ya Kidigitali

Kuwaunganisha watu na vitu kwenye intaneti



Kuwashirikisha watu wote

Kuhakikisha mawasiliano ya kidigitali yanapatikana kwa watu wote



Sayari yetu

Kupunguza athari kwa mazingira yetu

Tunaelekea Wapi

Dira yetu

- Kuwa kampuni ya kidigitali inayoongoza ambayo inanufaisha jamii iliyounganishwa kimtandao.
- Kuiuunganisha jamii kwa kesho iliyo bora.
- Kuwa mwajiri bora (Mahali bora pa kufanya kazi).

Kwa namna gani

Tunatekeleza kwa namna yetu

- Kuweza kuaminiwa na wateja
- Kujenga mustakabali
- Kujaribu – kujifunza haraka
- Kukamilisha mambo yote pamoja

Mkakati wetu ni upi

1 Kuthaminisha huduma ya data na fursa za kidigitali

2 Kuchochea ongezeko la wateja kupitia Huduma ya M-Pesa

3 Kuendelea kuimarisha huduma kwa wateja wa matumizi ya biashara kupitia bidhaa zetu mbalimbali

Tunahitaji kufanya nini


4 Kuwa chapa inayoongoza. Kushikilia na kuongeza umiliki wa soko

5 Kudhibiti gharama na kuwa na michakato yenye ufanisi

6 Watu. Vipaji bora, kuzingatia taratibu bora

Thamani tuliyojenga


Ufanisi wa kifedha



Kwa wanahisa wetu

Shilingi bilioni 54.5

zimepewa kama gawio kwa wanahisa wetu na kufikia jumla ya **Shilingi bilioni 121.8** zilizolipwa kwa miaka mitatu iliyopita




Kwa wateja wetu



milioni 15.5

Tumepanua wigo kwa wanaofikiwa na huduma zetu



Tumepanua mtandao wetu kwa kuongeza

Minara 460 – ya 4G
Minara 253 – ya 3G
Minara 201 – ya 2G

Tumeongeza huduma jumuishi za fedha kwa wateja wa M-Pesa zaidi ya

milioni 10.1

Tumetoa **Shilingi bilioni 52.0** katika mikopo – ya Songesha kwa wateja wetu

Kampuni ya **kwanza** katika Net Promoter Score (‘NPS’) tukiwa tunaongoza kwa alama 10

Kwa wafanyakazi wetu



Shilingi bilioni 57.7

zimetumika kwa wafanyakazi ikiwa ni pamoja na kuwapatia mafunzo ya kuendeleza ujuzi

Tuliendesha zoezi la kupima afya kwa hiari mara mbili ambapo

wafanyakazi 344

walihudumiwa

Katika jamii yetu

Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, tumechangia jumla ya **Shilingi trilioni 1.2** (2020: Shilingi bilioni 435, ongezeko la 11.1%) kwenye fedha za umma kwa njia ya kodi, tozo, masafa na tozo za mamlaka za udhibiti wa sekta.

Tunaunga mkono programu za Serikali za kufikisha mawasiliano vijijini, na kwa kipindi cha miaka nane iliyopita tumeshiriki kwa kujenga

minara 217

Shilingi bilioni 327.7

zimetumika kwa mwaka wa fedha 2020 kwa ajili ya malipo ya bidhaa na huduma za wasambazaji wa ndani na makampuni washirika zaidi 120 nchini Tanzania.

Zaidi ya **Shilingi bilioni 1.1**

zimetumika katika uwekezaji katika jamii, kukiwa na wanufaika zaidi ya **milioni 13.5¹** Tanzania

Zaidi ya ajira **135 000²** zisizo za moja kwa moja zilitolewa kwa watanzania.

1. Pamoja na shughuli za kijamii zilizofanyika moja kwa moja kwa wetu wa wateja.

2. Pamoja na wafanyabiashara huria (freelancers) na wakala wa M-Pesa.

Kuchukua hatua dhidi ya COVID-19

Kutekeleza Wajibu wetu kwa Jamii

Kwa kuzingatia dira ya kundi la makampuni ya Vodacom, lengo la Vodacom Tanzania ni **"Kuiunganisha jamii kwa kesho iliyo bora"**. Tukiwa ni kampuni ya kiteknolojia, tunatumia teknolojia na huduma za mawasiliano kuwaunganisha watu na kuziwezesha biashara katika ulimwengu unaokua kidigitali. Mawasiliano bora huongeza ubora wa maisha, huongeza ufanisi na kuwezesha kuishirikisha zaidi jamii kwa kuwezesha kubadilishana taarifa kati ya watu, jamii na biashara mbalimbali.

Katika kutekeleza lengo hili, Vodacom Tanzania imedhamiria kutekeleza Wajibu kwa Jamii, kwa kuzingatia kanuni tatu:



Kuhamasisha **tabia ya kuwajali** wateja wetu kupitia bidhaa za bei nafuu na rahisi kutumia zinazotolewa kwa ubora wa hali ya juu.



Kuhakikisha **usawa** na kuhamasisha ushirikishaji kidigitali, kwa kuongeza upatikanaji wa bidhaa, huduma na miundombinu ya kidigitali.



Kuonesha **na kungoza** ubunifu katika kusukuma mabadiliko kuelekea jamii ya kidigitali.


Katika kufanikisha lengo na wajibu wetu kwa Jamii, tumechukua jukumu muhimu la kutoa taarifa kuhusu jitihada zetu kupambana na COVID-19. Katika kupambana dhidi ya ugonjwa huu ulioenea duniani, tumechukua hatua mbalimbali kuhakikisha usalama wa wafanyakazi na makandarasu wetu, na kuendelea kuwaunganisha watu, biashara na Serikali katika mawasiliano.

- Tumeendelea kuwekeza ili kudumisha ubora na upatikanaji wa mtandao wetu kuhakikisha kuwa Serikali, biashara mbalimbali na wananchi wanaendelea kupata huduma za mawasiliano.
- Tumeendelea kuimarisha mfumo wa M-Pesa na huduma za kifedha kuwezesha malipo ya kielektroniki.
- Tumeunga mkono Serikali kwa kutoa msaada kwa vitengo muhimu vya Serikali, ikiwa ni pamoja na:
 - Kutoa mawasiliano ya intaneti bure kwa vikosi maalum vya Serikali, upatikanaji wa data bure kwa Taasisi ya Utafiti wa Tiba (NIMR), na data isiyo na ukomo kwa wafanyakazi wote katika vituo maalum vya kupambana na COVID-19.
 - Kuipatia Wizara ya Afya visambaza data na laini za simu kwa ajili ya data ili kuwezesha upatikanaji wa huduma ya intaneti bure kuharakisha mawasiliano na shughuli mbalimbali.
 - Kuchangia vifaa vyenye thamani ya Dola milioni 1 za Marekani (sawa na Shilingi bilioni 2.3) kupitia kitengo cha Vodacom Tanzania Foundation kuunga mkono juhudi za Serikali katika mapambano dhidi ya kuenea kwa ugonjwa huu.
- Tumeondoa tozo kwenye tovuti rasmi za Serikali zenye taarifa za COVID-19, na tumeanzisha kampeni kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, kuelimisha jamii kuhusiana na ugonjwa wa COVID-19.
- Tumewezesha wateja kufanya kazi wakiwa nyumbani, na kusaidia biashara ndogondogo kupitia upatikanaji wa vifurushi vya data, vifaa vya kuunganishia data (modem), na kutoa mafunzo jinsi ya kutumia vifaa vya kufanyia kazi nyumbani.
- Tumetoa fursa ya upatikanaji wa huduma ya elimu bure kwa wanafunzi wakati shule zilipokuwa zimefungwa, ikiwa ni pamoja na huduma kupitia mtandao kama vile 'Instant Schools' na 'Shule Direct'.
- Tumewaelimisha wananchi kuhusu COVID-19, tumetuma zaidi ya SMS milioni 110 kwa wateja milioni 15.5 kuhusu hatua za kiafya za kujikinga na tumetoa bure viungo vya kurasa za tovuti zenye maudhui ya COVID-19.


Juhudi hizi zimewezeshwa kwa kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha kunakuwa na usalama wa wafanyakazi na makandarasu, kuhakikisha kuwa sote tunatumia teknolojia ya kidigitali kupunguza maambukizi ya COVID-19 na kuwaunganisha watu kwa ajili ya maisha bora.

Vodacom Tanzania kwa ufupi

Mtandao wetu ulivyoenea



Kuwezesha jamii iliyonganishwa kimawasiliano



Bidhaa na huduma zetu

Tuna wateja zaidi ya milioni 15.5 wanaotumia bidhaa na huduma zetu.

| | |
|--|---|
| Sauti | Simu za kiganjani |
| Data | Modemu za broadband, intaneti kwa simu, mkongo, simu za kutumia waya |
| Ujumbe mfupi | Ujumbe mfupi wa maneno na programu za mitandao ya kijamii |
| Huduma zilizoongezwa thamani | Video kadiri ya mahitaji, kusikiliza muziki kuangalia video mbashara, muziki, michezo, bahati nasibu, habari, Huduma za mikopo ya muda wa hewani. |
| Huduma kwa wateja | Kituo cha mawasiliano, dawati la huduma kwa wateja, Maduka ya Vodacom, huduma binafsi (My Vodacom app, USSD code), huduma za kidigitali (kupitia mitandao ya kijamii, tovuti, WhatsApp na Live Chat app) na viashiria kwa wateja (ujumbe ibukizi) |
| Kuweka na kutoa fedha | Kwa wakala zaidi ya 107 000 |
| Kuhamisha fedha toka kwa mtu kwenda kwa mtu mwingine | Kutuma pesa ndani ya nchi na kimataifa (IMT) |
| Mifumo ya malipo ya kielektroniki | Kadi za kielektroniki "M-Pesa Mastercard", Mfumo wa malipo wa kulipa kwa Simu, Mteja kwenda kwenye Biashara ('C2B'), Biashara kwenda kwa Mteja ('B2C') na Biashara kwenda kwenye Biashara ('B2B') |
| Mifumo ya malipo ya kielektroniki | Akaunti ya akiba ya M-Pawa, M-Koba kwa ajili ya mikopo na kuweka fedha za kikundi, Akaunti ya akiba ya Halal Pesa ambayo inafuata miongozo ya Sharia na Huduma ya mkopo ya 'Songesha'. |
| Simu za kiganjani | Sauti, intaneti, ujumbe mfupi wa maneno, video |
| Uunganishaji | Pasi waya, kwa waya, VPN, mkongo, intaneti maalumu na ya kushirikiana |
| Managed mobility | Intaneti ya Vitu ('IoT'); APN kwa ajili ya makampuni |
| Usalama, cloud na Kuhifadhi (hosting) | |
| Bidhaa na huduma maalum | Huduma kwa wakulima 'Connected Farmer' au 'M-Kulima'; Huduma kwa mashule 'VodaShule', 'Connected education'. |

Huduma kwa matumizi ya wateja binafsi na kidigitali

M-Pesa

Matumizi ya wateja wa Biashara

Taarifa ya Mwenyekiti wa Muda

Huu umekuwa mwaka mwingine wenye changamoto za ushindani wa soko, kanuni mpya kutoka mamlaka za usimamizi, na mwishoni mwa mwaka tatizo la ugonjwa wa COVID-19 limeleta changamoto kubwa sana.

Margaret Ikongo



Utekelezaji wa miongozo mipya ya usajili wa wateja wote kwa alama za vidole, kwa kutumia Namba ya Kitambulisho cha Taifa (NIN) ulileta changamoto kubwa.

Makampuni ya huduma za simu pamoja na Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) na Wakala wa Vitambulisho vya Taifa (NIDA), tulizindua kampeni za kuelimisha jamii nchini kote mapema mwanzoni mwa mwaka huu wa fedha ili kuhakikisha utekelezaji unafanyika kabla muda haujaisha. Hata hivyo utekelezaji wa zoezi la usajili ulikuwa na changamoto kubwa hasa kutokana na watu wengi kutokuwa na Vitambulisho vya Taifa. Matokeo yake, wateja milioni 2.9 walifungiwa huduma katika robo ya mwisho ya mwaka wa fedha, ambapo kati ya hao, tulifanikiwa kuunganisha upya wateja 736 000. Kabla ya mwaka kuisha, ugonjwa wa COVID-19 uliingia nchini na ulileta changamoto mpya mbalimbali. TCRA ilisitisha zoezi la kuwafungia wateja kutokana na tatizo la ugonjwa huu.

Utekelezaji wa taratibu mpya za usajili wa wateja ulisababisha ongezeko la gharama ambazo zimefifisha picha halisi ya matokeo mazuri ya uendeshaji matokeo mazuri ya uendeshaji na utendaji mzuri wa kibishara. Tumeongeza wateja wapya milioni 1.4, hadi kufikia jumla ya wateja milioni 15.5 mwishoni mwa mwaka, na kuendelea kuongoza katika soko kwa kuwa na 31.9%¹ ya wateja wote wa soko. Mafanikio haya yalichochea na

shughuli za kibiashara zilizoendeshwa nchini kote, pamoja na uwekezaji wetu mkubwa katika miundombinu na mfumo wa usajili wa wateja. Zaidi ya Shilingi bilioni 20 zilitumika kuandaa mfumo wa usajili kujenga mtandao imara wa usajili wa wateja pamoja na gharama zilizotumika katika kusajili wateja kwa alama za vidole.

Ingawa shinikizo la kiudhibiti limeendelea kuwepo, tumewekeza Shilingi bilioni 154.6 katika mtandao wetu na miundombinu ya TEHAMA licha ya changamoto ya utekelezaji wa miongozo ya kiusimamizi kutoka Mamlaka husika, hii ni kuhakikisha wateja wetu wanafika na huduma bora na mtandao nchini kote. Ongezeko la 14.6% katika data linatokana na matokeo mazuri ya uendeshaji na utendaji mzuri wa kibishara wa uwekezaji katika mtandao wetu wa data, kuanzishwa kwa simu janja za gharama nafuu kwa bei ya Shi 45,000 na 48,000, na vilevile huduma nafuu za data. Imekuwa jambo la kutia moyo kuona huduma zetu za kibunifu za fedha zinaongezeka kwa mfano huduma za mikopo midogo, huduma za kutuma fedha kimataifa, malipo kwa wafanyabiashara na pia kuunganishwa kwa benki na watoa huduma wengine wengi katika mfumo wetu wa huduma za fedha kwa simu, M-Pesa. Tuna wateja milioni 10.1 wanaotumia huduma hii na tunaendelea kuongoza sekta hii hii tukiwa na 37.2%¹ ya wateja wote.

Tumewekeza
kwenye miundombinu yetu na TEHAMA

**Shilingi bilioni
154.5**

Tumetumia
**Shilingi bilioni
2.3**

katika kusaidia mapambano dhidi ya kuenea kwa ugonjwa wa COVID-19

1. Takwimu za mawasiliano za robo mwaka za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania za Machi 2020.

Ongezeko la 14.6% katika data linatokana na muendelezo wa uwekezaji katika mtandao wetu wa data.

Mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19 duniani umeleta changamoto kubwa sana kwa nchi, na shughuli zetu kama kampuni. Viongozi wetu watendaji walichukua hatua za haraka kuhakikisha usalama wa wafanyakazi, washirika wetu kibiashara na wateja, na kufanya kila kilichowezekana kuhakikisha wateja wanaendelea kupata huduma. Moja ya changamoto kuu iliyobaki ni mashambulizi ya kimtandao, hususan kutokana na wafanyakazi wanaofanya kazi wakiwa nyumbani kupitia mtandao, na pia ongezeko la mawasiliano katika mtandao. Uwekezaji tuliofanya ili kuongeza uimara wa mtandao umesaidia kupunguza changamoto hii kwa kiasi kikubwa. Tumeona fursa mbalimbali zilizojitokeza kutokana na mtandao wetu kuweza kuhudumia mahitaji yaliyoongezeka ya mawasiliano ya kidigitali, pamoja na huduma nyingine za ziada kama vile WhatsApp na jukwaa la mikutano la Zoom. Ongezeko hili la mahitaji linaonesha umuhimu wa kusudio letu la kuunganisha watu wengi zaidi kwenye ulimwengu wa kidigitali.

Kuhusu changamoto zinazojitokeza, Ripoti ya Mkutano wa Dunia kuhusu Changamoto za Kiuchumi "World Economic Forum's Global Risks Report" 2020 inasisitiza kuwa changamoto za kijiografia na kisiasa na makabiliano ya kiuchumi, kama vile vita vya kibiashara kati ya China na Marekani kwa miaka miwili iliyopita, havielekei kuisha. Sisi kama kampuni inayotegemea teknolojia ya

kidigitali na minyororo ya usambazaji duniani, hali hii inatishia usalama. Ingawa tumeona mafanikio mwishoni mwa mwaka uliopita katika 'Awamu ya Kwanza' ya mkataba wa kibiashara kati ya Marekani na China, bado hii inabaki kuwa changamoto ambayo tutaendelea kuifuatilia.

Mazingira ya kiusimamizi bado yanabaki kuwa changamoto nchini Tanzania. Mwaka uliopita, kanuni kadhaa zilitangazwa, ambazo utekelezaji wake unaweza kuathiri huduma za fedha na mawasiliano kwa wateja. Bodi inachukua tahadhari na kuzipa umuhimu unaostahili changamoto hizi kwa kufuatilia kwa karibu na kushirikiana na Mamlaka za Usimamizi na wadau wengine kujadili namna ya kuzitatuwa na au kupunguza madhara. Katika miezi yangu michache nikiwa Mwenyekiti wa muda, nimefurahishwa kuona tunapokea maoni mazuri kutoka kwa wadhibiti wetu na maafisa wa serikali kuhusu mahusiano mazuri ya Vodacom Tanzania na wadau wake, ambayo ninaamini yamechochewa na Kampuni kudumisha nidhamu ya hali ya juu.

Kazi yangu kama Mwenyekiti wa Muda wa Bodi ya Wakurugenzi ni kuhakikisha kuwa sisi kama Bodi, tunafanya kazi ya utumishi makini, kusimamia utendaji wa Kampuni na mwelekeo wa kimkakati na kuhakikisha kuwa timu ya viongozi watendaji inatekeleza wajibu wake kwa uaminifu na uwajibikaji. Kabla ya kuchukua nafasi ya Mwenyekiti wa Muda, nilikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji, nikiwa mtaalamu wa masuala ya usimamizi wa bima na dharura. Hii iliniwezesha kutekeleza jukumu langu la usimamizi wa utawala, utekelezaji na dharura, wakati ambapo sekta inasimamiwa kwa kiwango cha juu. Ninaamini kuwa tuna bahati kuwa na Bodi ambayo ina mchanganyiko wa watu wenye ujuzi, uzoefu na sifa mbalimbali zinazohitajika ili kudumisha utamaduni imara wa uwajibikaji, pamoja na uongozi na usimamizi ili kuhakikisha malengo ya wadau yanafikiwa. Kiutendaji, tumekuwa na mwaka mzuri na kamati za Bodi yetu zimefanya kazi nzuri kutoa mwongozo kwa menejimenti. Mabadiliko ya mkaguzi wa nje Ernst & Young, yameenda vizuri.

Mazingira ya kibiashara yameendelea kuwa ya ushindani. Wakati baadhi ya washindani wakiendelea kuleta msongo katika bei Vodacom Tanzania imebaki kuwa makini katika kuwapatia wateja huduma zenye ubora kupitia uwekezaji mkubwa na

endelevu katika mtandao. Tutaendelea kuongoza katika ubunifu na soko na tutavuta a watu wengi zaidi kwenye ulimwengu wa kidigitali, kwa kupitia huduma za fedha, kupanua huduma zetu kwa matumizi ya wafanyabiashara, kulenga kupunguza gharama, na vilevile kuhakikisha tunadumisha mtandao mpana zaidi hapa nchini. Ili kufanikisha haya, mi muhimu kuwekeza kwenye rasilimali watu kuhakikisha kila wakati tuna wafanyakazi wanaotosheleza mahitaji ya kiutendaji. Tutaendelea kuwawezesha wateja wetu kutatua matatizo yanayohusu huduma kwa kupitia njia mbalimbali za kujihudumia bila yakuwasilina na watoa huduma, na kuhakikisha wateja wanajisikia kuwa washirika muhimu kwetu.

Uwekezaji wetu katika mtandao unaendelea kutupatia uwezo wa kiushindani na unatuwezesha kutekeleza wajibu wetu wa kutumia masafa ya 700 MHz ambayo tumeyanunua mnadani miaka miwili iliyopita kwa ahadi ya kuongeza mawanda ya huduma ya 4G. Tutaendelea kushirikiana na Serikali katika utekelezaji makini wa hatua za kupambana dhidi ya kuenea kwa ugonjwa wa COVID-19. Vodacom Tanzania Foundation, inayojulikana kutokana na kazi yake ya uwekezaji kwa jamii, ilichukua hatua za haraka kwa kutoa mchango wa Shilingi bilioni 2.3 kuunga mkono juhudi za serikali.

Ni heshima kubwa kutumikia kama Mwenyekiti wa Muda wa Bodi, nafasi ambayo nimechukua kufuatia kujiuzulu kwa Ndugu Ali A. Mufuruki, kuanzia tarehe 1 Desemba 2019. Nilisikitika sana kusikia kuhusu kifo chake; alikuwa kiongozi mahiri, muadilifu na mwenye upendo, atakumbukwa daima. Kwa niaba ya Bodi, ninapenda kutoa shukrani zetu kwa timu ya viongozi wa Vodacom Tanzania na wafanyakazi wote wa Kampuni kwa kujituma kwao kipindi hiki chenye changamoto kubwa kwa kuhakikisha wateja wetu wanaendelea kupata huduma za mawasiliano. Pia ninapenda kutoa shukrani zangu kwa Hisham Hendi kwa uongozi wake shupavu, kufanya maamuzi mazuri na kusimamia utekelezaji madhubuti. Ninapenda pia kuwashukuru Wakurugenzi wote ambao wamefanya kazi nae tangu nilipochukua nafasi hii kama kiongozi wa muda.



Margaret Ikongo
Mwenyekiti wa Muda
14 Julai 2020

Taarifa ya Mkurugenzi Mtendaji

Mwaka huu tumepata mafanikio katika uendeshaji jambo ambalo limeleta msukumo wa kibiashara, yakidhihirishwa na sisi kuendelea kuongoza katika soko la wateja kwa 31.9%¹. Tumewekeza Shilingi bilioni 154.6 katika mtandao na miundombinu ya TEHAMA ili kuhakikisha kuwa wateja wote wanapata huduma bora na mtandao nchini kote. Kupitia jitihada hizi, wateja milioni 1.4 wamejiunga na mtandao unaoongoza wa Vodacom Tanzania, ongezeko la 9.8% hadi wateja milioni 15.5², wanapata huduma mbalimbali za kifedha na kidigitali, licha ya kuwepo shinikizo la kiusimamizi na kiushindani.

Hisham Hendi



Tumeridhishwa na mafanikio ya mikakati iliyochukuliwa mwaka ulioisha iliyolenga kuhakikisha kuwa tunafuata miongozo ya namna ya kusajili wateja wapya. Tumetumia zaidi ya Shilingi bilioni 20 kuanzisha mfumo wa usajili pamoja na kuhakikisha tunakuwa na mtandao bora nchini wa kusajili wateja, tukiwa na vituo vya kuhudumia wateja zaidi ya 35,000. Hadi Machi 31, 2020, robo tatu ya wateja wetu walikuwa tayari wamekamilisha usajili kwa kutumia alama za vidole. Jumla ya wateja milioni 2.9 walifungiwa huduma, lakini kati yao, 736 000 waliunganishwa tena kwenye mtandao, na wateja wengine milioni 2.5 bado hawajakamilisha usajili kwa alama za vidole kwa mujibu wa muongozo. Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) imesitisha kwa muda zoezi la kufungia wateja huduma kutokana na janga la COVID-19.

Kwa mwaka huu, tumepata ongezeko la mapato la 0.9% (1.8% bila kuzingatia athari za viwango vya maingiliano ya mitandao), matumizi ya M-Pesa na data yakiongoza ukuaji. Mafanikio haya yametokana na utekelezaji na ufanisi wa mikakati isiyotetereka na bora. Athari za kifedha zilizosababishwa na kutekeleza mwongozo wa usajili wa wateja zimefifisha uhalisia wa mafanikio yetu kiutendaji. Ushahidi unaweza kuonekana kwenye kupungua kwa mapato ya huduma katika nusu ya pili ya mwaka, pamoja na kupanda kwa gharama za utekelezaji wa mwongozo.

Mafanikio katika utekelezaji wa mikakati yetu

Kwa ujumla tulipata ongezeko la mapato katika maeneo yetu ya msingi ya kimkakati, huku mapato ya data yakiongezeka kwa 9.8% na M-Pesa kwa 7.4%. Tumeendelea kutoa huduma bora za data zenye kiwango cha juu sana nchini na hivyo kupungua pengo la kidigitali tukiweshwa na uwekezaji endelevu katika miundombinu, kuingiza sokoni simu janja za bei nafuu na huduma nafuu za data. Katika mwaka uliopita tuliongeza minara 460 ya 4G na minara mingine 253 ya 3G, na kuingiza sokoni simu za 'Smart Kitochi' zinazouzwa kwa gharama nafuu kati ya Shilingi 45 000 na 48 000 tu, zinazowawezesha wateja kupata huduma bora ya data. Hii mesababisha ongezeko la matumizi ya huduma ya data kwa 14.6%, hususan kupitia mtandao wa 4G.

1. Takwimu za mawasiliano za robo mwaka za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania za Machi 2020.

2. Wateja hujumuisha jumla ya watumiaji wote wa huduma katika mtandao kwa kipindi cha miezi mitatu iliyopita. Hii inajumuisha wateja wa huduma ya malipo baada ya matumizi, ambao hulipa gharama za kuunganishwa kila mwezi. Hawa wanajumuishwa bila kujali kama walitumia huduma katika mwezi husika, na pia wateja waliotumia huduma wakati wakizuru nchi nyingine. Kulikuwa na wateja milioni 11.9 waliotumia huduma za mtandao katika kipindi cha mwezi mmoja uliopita.

Athari za COVID-19 na hatua tulizochukua

Kuenea kwa janga la ugonjwa wa COVID-19, ambao ulipamba moto mwanzoni mwa mwaka 2020, ulisababisha misukosuko isiyotegemewa duniani kote, kufunga sekta za uchumi, kuvuruga minyororo ya usambazaji, na kuwafanya watu wengi kukosa kazi. Tumeona changamoto kubwa katika sekta ya hoteli na utalii nchini Tanzania na kulegalega kwa ukuaji wa uchumi, na kupungua kiujumla kwa matumizi ya bidhaa. Ingawa nchi yetu haikuchukua hatua za kuzuia na kufunga kabisa shughuli za kiuchumi na kijamii, kupungua mikusanyiko isiyo na lazima, kufungwa kwa mashule na kupungua kwa shughuli za kila siku kutokana na watu kushauriwa kufanya kazi wakiwa majumbani, kulileta fursa na changamoto katika biashara. Moja ya fursa hizo ni ongezeko la mahitaji ya intaneti katika biashara na kwa wateja wanaofanya kazi nyumbani.

Tulikuwa moja ya kampuni za kwanza kuwaomba wafanyakazi wafanye kazi wakiwa majumbani, tulichukua hatua madhubuti kuhakikisha kunakuwa na usalama wa wafanyakazi, kuwaunganisha kidigitali na kuendeleza shughuli za biashara. Kupitia Vodacom Tanzania Foundation, tumechangia jumla Shilingi bilioni 2.3 kuunga mkono juhudi za serikali kupambana na COVID-19. Tumefanya kampeni za kuelimisha jamii kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, ikiwa ni pamoja na kutoa huduma za bure za ujumbe mfupi wa maneno kuhusu COVID-19, kuondoa tozo kwenye baadhi ya tovuti rasmi za serikali zenye taarifa kuhusu COVID-19 na kutoa vifurushi maalum vya data kwa wafanyakazi wanaotoa huduma za afya. Lengo letu kuu lilikuwa kuhakikisha wateja wetu wanaendelea kuunganishwa, na mashirika katika sekta binafsi na sekta ya umma yanaendelea kufanya kazi kwa ufanisi bila wafanyakazi kwenda maofisini.

Sehemu muhimu ya mkakati wetu ilikuwa kuanzisha vifurishi vya kuvutia vya data, uingizaji sokoni wa simu janja, ikijumuisha kampeni shirikishi na wabia wetu kuhusu matumizi ya simu janja zikiwalenga hususan vijana na wateja wenye matumizi makubwa. Tuliendelea kuboresha zaidi mtandao wetu, na kuwekeza katika kuongeza uwezo wetu wa kuhudumia na kujenga uwezo wa kuhimili mtikisiko.

Huduma yetu ya M-Pesa inaendelea kutekeleza lengo lake la kuwawezesha watu wengi iwezekanavyo kutumia huduma zetu za kifedha kwa wepesi huku ikichangia ukuaji wa uchumi. Katika mwaka uliopita tulikuwa na wateja³ milioni 10.1, waliofanya miamala bilioni 1.4 yenye thamani ya Shs trilioni 58.1. Tulitana wigo na kuongeza huduma mpya zikiwemo za mikopo midogomidogo, kutuma na kupokea pesa kutoka nchi za nje, kuunganishwa na mifumo ya kibenki na wadau wengine. Huduma yetu ya mkopo ijulikanayo kama 'Songesha' imeonesha mafanikio makubwa kwa kuwawezesha wakopaji wadogowadogo milioni 5.3 kukopa hadi Shs 70,000, huku mikopo yenye thamani ya Shs bilioni 52.0 ilitolewa katika kipindi hiki cha mwaka. Tuna mpango wa kuisambaza huduma ya Songesha kwa mawakala wa M-Pesa. Kwa kushirikiana na kampuni za TerraPay na World Remit, tulishuhudia ongezeko mapato yatokanayo na huduma ya kutuma na kupokea fedha kati ya Tanzania na nchi za nje kwa kiwango cha tarakimu mbili. Wateja wa huduma hii sasa wanaweza kutuma na kupokea fedha kupitia M-Pesa. Tumepokea miamala yenye thamani ya Shs bilioni 115.6, kati ya hizo Shs bilioni 48.6 zilitumwa ndani ya ukanda ya Afrika Mashariki.

Kitengo chetu kinacho hudumia wateja wa matumizi ya kibishara pia kilifanya vizuri, na kumekuwa na ongezeko kubwa la huduma za simu za kiganjani na zisizohamishika. Tumefanya tafiti juu ya huduma ya intaneti ya vitu (IoT) ikiwa ni maandalizi ya kuleta huduma bora zaidi katika eneo hilo. Kwa kushirikiana na kampuni ya Mezzanine tumeandaa na kuingiza sokoni bidhaa yetu ijulikanayo kama 'Connected Farmer' ambayo imeleta mageuzi makubwa kwenye sekta ya kilimo ikiwa na wakulima zaidi ya 10,000 waliojiunga. 'Connected Education' na 'VodaShule' ni mifumo iliyorahisisha mifumo ya uendeshaji na malipo mashuleni.

Katika mazingira yaliyopo ya ushindani mkali, ni jambo la kufurahisha kuona kuwa tumeendelea kuwa mtoa huduma ambaye ni chaguo la kwanza la wateja kama tathmini za ubora wa mtoa huduma (Net Promoter Score, NPS) ilivyothibitisha. Katika mwaka huu wa fedha tulipata alama 53 ikiwa ni tofauti ya alama 10 kati yetu na mshindani anayetufuata. Hii ni uthibitisho wa ubora wa mtandao wetu, mfumo wa M-Pesa, mafanikio ya kampeni zetu na uwiano mzuri kati ya tozo na ubora wa bidhaa zetu, na tija katika mikakati ya kumfikia mteja.

Tumeendelea kuweka mazingira ya kuvutia kwa wafanyakazi wenye vipaji hapa nchini. Mwaka huutumeteua Watanzania wanne kuwa wakurugenzi wapya na hivyo kuongeza uwakilishi wa wazawa kwenye Kamati ya Viongozi Watendaji kufikia 69%. Kama sehemu ya mageuzi ya kidigitali, tumeunda idara mpya itakayolenga kuendeleza huduma za kidigitali. Na pia, kutokana na ongezeko la changamoto za kujiendesha kadiri ya miongozo ya wasimamizi, tumeimarisha uwezo wa idara yetu inayosimamia uthabiti wa utekelezaji wa miongozo ikiwa njia ya kuepuka madhara ya kukiuka miongozo ya wasimamizi.

Tumeendeleza lengo la kuvumbua miundo, kanuni na zana nyumbufu katika shughuli za uendeshaji. Ili kuimarisha dhamira yetu ya kuiunganisha jamii kuifikia kesho iliyo bora, tumezindua kauli mbiu ya 'Spirit of Vodacom' kwa madhumuni ya kuingiza utamaduni wa kumjali mteja jambo linalotoa msukumo katika ubunifu na ubia. Mwishoni mwa mwaka tuliingia ubia na kampuni ya Smart Lab ili kuendesha na kusimamia programu yetu mpya ya 'Digital Accelerator'. Ni imani yetu kuwa mkakati huu utasaidia kukuza zaidi ya biashara 1,000 zinaoanza na kuziwezesha kuzalisha faida, kwa kuunganishwa katika mfumo wetu wa huduma za fedha kwa simu. Katika mwaka wa kwanza wa programu hii, tuliwekeza zaidi ya Shilingi milioni 350 na hadi sasa tuna orodha ya wajasiriamali 15 watakaokuwa chini ya usimamizi wa watalaamu wetu.

Mazingira magumu ya uendeshaji

Utendaji wetu unaoridhisha umefikiwa katika mazingira yenye changamoto za tekelezaji wa miongozo ya usimamizi na uhibitaji wa soko lenye mazingira ya ushindani mkubwa

na kupungua kwa matumizi ya wateja. Soko letu ni mojawapo ya masoko yenye viwango vya chini zaidi vya bei za data barani Afrika. Mazingira haya yamechajizwa na ushindani mkali katika bei, ambapo baadhi ya wadau wanalenga ongezeko la muda mfupi la wateja badala ya maslahi endelevu na ya muda mrefu.

Mojawapo ya changamoto kubwa ya kiusimamizi kwa mwaka huu ni ile inayohusu utekelezaji wa mwongozo mpya wa TCRA katika kusajili laini za simu unaotaka usajili wa laini ufanyike kwa kutumia alama za vidole na Namba ya Kitambulisho cha Taifa. Mchakato huu ulianza Mei 2019 na kutarajiwa kumalizika Desemba 2019, ambapo muda uliongezwa hadi Januari 2020. Changamoto nyingine inahusiana pia na kanuni mpya ya umiliki wa laini za simu ambapo mteja ataruhusiwa kumiliki laini moja tu kwa kila kampuni ya simu kwa matumizi ya sauti, data na ujumbe mfupi. kuanzia Julai 1 2020. Kibali cha TCRA kitahitajika iwapo mteja atahitaji kumiliki zaidi ya laini moja ya simu. Vodacom inaendelea kuwasiliana na TCRA kwa lengo la kupata mfumo unaojiendesha wenyewe ili kila mteja aweze kuomba kumiliki laini ya simu ya ziada. Kwa upande wa M-Pesa, Benki Kuu ilichapisha kanuni mpya za kumlinda mlaji wakiwemo wateja wa M-Pesa. kanuni zimeweka aina mbalimbali za makatazo kwa watoa huduma za kifedha, zikiwemo benki, na watoa huduma za fedha kielektroniki. Tunaendelea kuwasiliana na Benki Kuu ya Tanzania kupitia Chama cha Watoa Huduma za Simu Tanzania ili kupata ufafanuzi wa utekelezaji wa kanuni hizo.

Mtazamo Wetu Kimkakati

Mtazamo wetu wa siku zijazo ni kwamba ushirikiano endelevu na TCRA na NIDA utawawezesha wateja waliofungiwa laini zao kurudishiwa huduma hiyo katika kipindi kifupi iwezekanavyo, na kuongeza kasi ya usajili kwa alama za vidole kwa wateja waliobaki.

Tutaendelea kuweka mkazo katika kuongeza thamani ya huduma zetu kwa kutoa huduma na bidhaa muafaka kwa wateja wetu, huku tukiendelea kuwezesha upatikanaji wa simu janja za bei nafuu na kuendeleza uwekezaji katika mtandao. Tumeboresha huduma zetu za kidigitali kwa lengo la kuwapa wateja wetu wigo mpana zaidi wa huduma kwa kupitia mifumo ya kidigitali sambamba na kuongeza

3. Wateja wa M-Pesa hujumuisha wateja wote waliofanya miamala iliyochajwa gharama za huduma, katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita. Kulikuwa na wateja milioni 6.7 waliotumia huduma za mtandao katika kipindi cha mwezi mmoja uliopita.

Taarifa ya Mkurugenzi Mtendaji inaendelea

vyanzo zaidi vya mapato. Tutaendelea kuongeza kasi ya safari yetu ya mageuzi ya kidigitali kupitia huduma mbalimbali za ziada. Janga la COVID-19 limeongeza kasi ya mageuzi yetu ya kidigitali kwa kiwango kikubwa sana.

Jukwaa letu la M-Pesa linatoa fursa nyingi za ongezeko la ukuaji, hususan tunapotoa huduma za ziada ikijumuisha huduma kwa matumizi ya kibiashara, huduma za kifedha na biashara kwa simu. Tutaendelea kuweka kipaumbele cha kufikisha huduma za fedha kwa watu wengi zaidi kwa kupanua huduma za M-Pesa kwa wateja wetu. Tutatumia nafasi yetu ya kuwa mtoa huduma anayeongoza soko kufungua fursa zinazoambatana na teknolojia mpya.

Mwaka ujao, tutajikita pia katika huduma kwa wateja wa matumizi ya kibiashara. Kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali, tunadhamiria kuimarisha huduma za mfumo wa IoT. Pia, tutaendelea kuimarisha na kuthaminisha huduma zetu mpya ikiwemo 'Connected Farmer' ambayo inaleta mapinduzi ya kidigitali katika kuboresha kilimo nchini kwa ushiriano na Wizara ya Kilimo.

Kupitia programu yetu ya kuendeleza vipaji vya kidigitali, tutaimarisha nafasi yetu ya kuongoza katika suala la ubunifu kwa kuongeza ubia na ufadhili kwa wabunifu ambao wana mawazo mazuri lakini hawana mtaji wa kuwawezesha kutumia ubunifu huo katika kufaidika kibiashara.

Mikakati hii itaambatana na hatua mbalimbali kwa lengo la kulinda hadhi ya nembo zetu za kibiashara, kuendesha shughuli kwa tija, kuhakikisha muda wote tuna wafanyakazi wenye ujuzi stahiki, uwezo na tabia zitakazo iwezesha kampuni kuifikia ndoto ya ya kuwa kampuni kinara kidigitali.

Janga la COVID-19 linatarajiwa kuwa litaathiri uchumi wa ndani na kupunguza uwezo wa kifedha wa wateja. Ukubwa wa athari utategemea matukio ya siku za usoni, na mengi kati ya hayo bado ni vigumu kuyatabiri. Tutaendelea kufuatilia na kupima uwezekano wakutokea athari hizo pamoja na kuchukua nafasi muhimu katika kuisaidia serikali na wateja wetu ili tuvuke salama kipindi hiki kigumu.

Shukrani

Katika kuhitimisha, ningependa kuwashukuru viongozi wenzangu kwenye Bodi na watendaji, wafanyakazi wote wa kampuni kwa kuniunga mkono, kutoa ushauri na moyo wa kujitoa. Ningependa pia kumshukuru kwa dhati mwenyekiti wa Bodi aliyepita, marehemu Ali A Mufuruki kwa moyo wa kujitolea na uongozi uliotukuka. Kwangu, imekuwa heshima kubwa kuwa katika mwaka wa pili kama Mkurugenzi Mkuu wa Vodacom Tanzania. Sina shaka miaka ijayo itakuwa ya kusisimua iwapo tutafanya kazi kwa kushikamana katika kufanikisha uwezo wa utekelezaji wa ahadi zetu kwa wadau mbalimbali, na kuiingiza Tanzania katika zama za kidigitali.



Hisham Hendi
Mkurugenzi Mkuu
14 Julai 2020



Ufanisi wetu kifedha

| Taarifa za Jumla | 2020 | 2019 | % ya mabadiliko mwaka hadi mwaka |
|---|------------------|-----------|----------------------------------|
| Mapato ya huduma (Sh milioni) | 1 024 916 | 1 016 237 | 0.9 |
| Ambapo | | | |
| Mapato ya huduma za simu kwa sauti | 373 005 | 385 498 | (3.2) |
| Mapato ya M-Pesa | 358 243 | 333 519 | 7.4 |
| Mapato ya data za simu | 180 840 | 164 658 | 9.8 |
| Mapato ya simu zinazozingia | 53 204 | 65,709 | (19.0) |
| Mapato ya Ujumbe mfupi wa maneno | 42 413 | 41 441 | 2.3 |
| Jumla ya mapato | 1 032 667 | 1 024 587 | 0.8 |
| Mapato kabla ya riba, kodi na uchakavu (EBITDA) (Sh milioni) | 364 763 | 288 657 | 26.4 |
| Kiwango cha EBITDA (%) | 35.3 | 28.2 | 7.1ppts |
| Gharama za uwekezaji | (154 586) | (171 432) | 9.8 |
| Asilimia ya gharama ya uwekezaji ¹ | (15.0) | (16.7) | 1.8ppts |
| Nafasi yetu kwa idadi ya wateja wa soko ² | Kwanza | Kwanza | |
| Idadi ya wateja hai/amilifu ³ (maelfu) | 15 513 | 14 133 | 9.8 |
| Wateja hai/amilifu wa data ⁴ (maelfu) | 7 687 | 7 892 | (2.6) |
| Dakika zilizotumika kwa mwezi ⁵ | 172 | 172 | (0.2) |
| Wastani wa kipato kutoka kwa mteja ARPU ⁶ (Shilingi kwa mwezi) | 5 616 | 6 010 | (6.6) |
| Idadi ya wafanyakazi | 551 | 548 | 0.5 |
| Idadi ya minara | | | |
| 4G | 1 321 | 861 | 53.4 |
| 3G | 2 682 | 2 429 | 10.4 |
| 2G | 3 225 | 3 024 | 6.6 |
| Ulinganishi wa NPS ⁷ (nafasi kulingana na washindani) | Kwanza | Kwanza | |

Maelezo:

- Matumizi ya gharama za uwekezaji kama asilimia ya mapato.
- Kwa mujibu wa takwimu za mawasiliano za robo mwaka za Mamlaka ya Mawasiliano za Machi 2020
- Walaji wanaotumia huduma wanatokana na jumla ya idadi ya watumiaji simu waliotumia huduma yoyote katika miezi mitatu iliyopita. Hii ni pamoja na wateja wanaolipa ada ya kila mwezi ambayo inawapa haki ya kutumia huduma husika hata kama kiuhalisia hawaitumii huduma hiyo na wale wateja ambao wanawasiliana nje ya mtandao.
- Wateja hujumuisha jumla ya watumiaji wote wa huduma katika mtandao kwa kipindi cha miezi mitatu iliyopita. Hii inajumuisha wateja wa huduma ya malipo baada ya matumizi, ambao hulipa gharama za kila mwezi kupata haki ya kutumia huduma husika. Hawa wanajumuishwa bila kujali kama walitumia huduma katika mwezi husika, na pia wateja waliotumia huduma wakati wakizuru nchi nyingine.
- Dakika za matumizi kwa mwezi hukokotolewa kwa kugawanya jumla ya dakika zilizotumika kwa mwezi kwa wastani wa watumiaji wa dakika hizo katika kipindi hicho.
- ARPU inakotolewa kwa kugawa wastani wa mapato ya huduma kwa mwezi kwa wastani wa jumla ya wateja kwa mwezi katika kipindi hicho.
- Net promoter score (NPS) ni kipimo kuanzia -100 hadi 100 ambacho kinaonesha utayari wa wateja kupendekeza bidhaa au huduma za mtoa huduma kwa watu wengine. Inatumika kama kigezo cha kupima hali ya kuridhika kwa wateja na bidhaa au huduma za mtoa huduma imani ya wateja kwa chapa hiyo. Kwa kila mtoa huduma, majibu yanakusanywa kutoka kwa wateja ambao wanatumia bidhaa au huduma zake kama njia kuu au mbadala ya mawasiliano ya simu (mtumiaji mkuu au mtumiaji mbadala). Majibu kutoka kwa watumiaji wakuu na watumiaji mbadala yanalinganishwa/pimwa kwa uwiano asilia wa watumiaji wakuu na watumiaji mbadala wa mtoa huduma huyo ili kukokotoa NPS.

Mapato

- Mapato ya huduma** yaliongezeka kwa 0.9% (1.8% ukiondoa athari za mabadiliko katika gharama inayotozwa kwa kila dakika ya simu kwenda/kutoka mitandao mingine ya ndani – MTRs) hadi Shilingi bilioni 1 024.9 ukuaji ukisababishwa na ongezeko la 3.3% katika mapato ya matumizi ya wateja. Ongezeko hili lilitokana na ongezeko kubwa la wateja la 9.8%, likisawazishwa kwa kiasi na kushuka kwa wastani wa matumizi kwa mteja (ARPU) kutokana na kufungiwa huduma kwa wateja milioni 2.9 ambao laini zao za simu hazikusajiliwa kwa alama za vidole, pamoja na shinikizo la ushindani mkubwa wa bei. Tumeridhishwa na ongezeko la wateja milioni 1.4 katika mwaka huu, lilitokana na shughuli za kibiashara zilizofanywa sehemu mbalimbali nchini na kwa kiasi fulani kuchochewa na wateja waliopo sasa ambao wamesajili laini mpya za simu badala ya kusajili laini za simu ambazo tayari wanazo hivi sasa.
- Mapato ya huduma za simu kwa sauti** yalipungua kwa 3.2% hadi Shilingi bilioni 373.0, na kusababisha kupungua kwa mchango wake katika mapato ya huduma kwa pointi 1.5 hadi 36.4%. Kiwango cha kushuka kiliongezeka katika nusu ya pili ya mwaka kutokana na kupungua kwa shughuli za wateja kufuatia utekelezaji wa kufungiwa huduma wateja wasiokamilisha usajili wa laini zao za simu kwa alama za vidole, na vilevile ongezeko la shinikizo la ushindani wa bei.
- Mapato ya M-Pesa** yaliongezeka kwa 7.4% hadi Shilingi bilioni 358.2, na mchango wake kwenye mapato ya huduma kuongezeka kwa pointi 2.2 hadi 35.0%. Ongezeko la matumizi ya huduma ya M-Pesa kwa wateja wetu lilichagizwa na ongezeko la wastani wa kipato kutoka kwa mteja (ARPU), huku likisawazishwa kwa kiasi na wateja kupunguza matumizi katika nusu ya pili ya mwaka kufuatia utekelezaji wa kufungiwa laini za simu zisizokamilisha usajili kwa alama za vidole na shinikizo linaloendelea la ushindani wa bei. Kwa

Ufanisi wetu kifedha inaendelea

sasa wateja milioni 10.1 wanatumia huduma hii na tunaendelea kuongoza katika sekta ya huduma ya fedha kwa kutumia simu kuwa na 37.2% ya wateja wote. M-Pesa inatekeleza ahadiyake ya kuwashirikisha na kuwawezesha wateja kufanya miamala kwa urahisi na kuchangia katika ukuaji wa uchumi. Jumla ya miamala bilioni 1.4, yenye thamani ya Shilingi trilioni 58.1 imefanyika kupitia mfumo wa fedha kwa simu katika mwaka huu, ikiwa ni ongezeko la 21.1% la thamani ya miamala. Huduma yetu ya 'Songesha' inaendelea vizuri, kukiwa na wateja milioni 5.3 wanaotumia huduma hii, na Shilingi bilioni 52.0 za mkopo zikiwa zimetolewa kwa mwaka huu. Tumepanua huduma yetu ya kutuma na kupokea fedha kutoka nje ya nchi kwa kushirikiana na washirika wetu wa kimataifa, ikiwa ni pamoja na TerraPay na WorldRemit, na kupokea jumla ya Shilingi bilioni 115.6 katika mfumo huu na kutuma Shilingi bilioni 48.6 ndani ya ukanda wa Afrika Mashariki.

- **Mapato ya data za simu** yaliongezeka kwa 9.8% hadi Shilingi bilioni 180.8, hasa kutokana na ongezeko la 14.6% la matumizi ya data, likisababishwa na ongezeko kubwa la matumizi katika teknolojia ya 4G, jambo ambalo linaonesha uhitaji wa huduma za data kwa simu ni mkubwa. Ongezeko hili ni matokeo ya uwekezaji endelevu katika huduma ya data pamoja na kuwawezesha upatikanaji wa simu janja za gharama nafuu na huduma nafuu za data. Wateja wa data wamepungua kwa 2.6% hadi milioni 7.7, hasa kutokana na kufungiwa huduma kwa wateja ambao laini za simu hazikusajiliwa kwa alama za vidole zoezi ambalo lilifanyika katika robo ya mwisho ya mwaka.
- **Mapato ya simu zinazolingia** yalishuka kwa 19.0% hadi Shilingi bilioni 53.2, yakiakiisi punguzo la 50% ya gharama kwa dakika inayotozwa kwa simu zinazotoka katika mitandao mingine ya ndani lililofanyika mwezi Januari 2020 kulingana na utaratibu uliowekwa na msimamizi wa sekta ya mawasiliano. Kwa kiasi fulani athari za kupunguzwa tozo, zimefidiwa na ongezeko la 30.1% la idadi ya dakika za simu zinazolingia, kwa kuwa watoa huduma wameendelea kuongeza kiasi cha dakika kwenda mitandao mingine katika ofa zao. Tumeendelea kushuhudia kushuka kwa mchango wa mapato ya simu zinazolingia katika mapato ya huduma, ambapo kwa sasa yameshuka hadi kufikia 5.2% (pungufu kwa 1.3ppts).
- **Mapato ya ujumbe mfupi** yameongezeka kwa 2.3% hadi Shilingi bilioni 42.4, ambapo idadi ya jumbe zilizotumwa zikiwa zimepungua kwa 3.5% hadi bilioni 33.1, wakati bei kwa kila ujumbe imeongezeka kwa 6.0%. Hii ni kutokana na kuendelea kufanya uboreshaji katika ofa zetu na marekebisho ya bei.

Elewa athari za matumizi ya kanuni ya 'IFRS 16'

Kanuni ya uandaaji na uwasilishaji wa taarifa ya 'IFRS 16'; Gharama za kukodi, zilichukua nafasi ya kanuni ya awali ya 'IAS 17', ambapo chini ya 'IAS 17', mikataba ya ukodishaji iliainishwa kama gharama ya kiuendeshaji au ya mikopo ya kifedha. Chini ya 'IFRS 16', mikataba ya namna hiyo inatambuliwa kama 'haki ya kutumia mali', ikionesha haki ya kutumia mali iliyokodishwa, na wajibu wa kulipia pango siku za baadaye kwa muda wa mkataba, pamoja na muda wa ziada ambao Kampuni ina fursa ya kuongeza mkataba.

Utaratibu wa kuripoti mali iliyokodishwa katika kanuni ya 'IFRS 16' ni sawa na kuripoti ukodishaji mali kwa muda mrefu (finance lease) chini ya utaratibu wa 'IAS 17'; ambapo gharama za ukodishaji zinaripotiwa kama gharama za uchakavu wa mali iliyokodishwa (depreciation) na riba katika deni la pango, ambao linakadiriwa katika thamani ya sasa kwa kutumia kiwango cha riba cha kampuni, ingawa kiwango cha riba kinadokezewa katika mkataba wa kukodisha, kiwango kinachotumika kinatumia wakati kimedhihirika. Malipo ya riba kwa

kawaida yatakuwa makubwa katika hatua za awali na yatapungua muda wa mkataba unavyoenda.

Matumizi ya 'IFRS 16' yamesababisha kutambuliwa katika vitabu vya fedha, mali zilizokodishwa na madeni ya pango kuhusiana na ukodishaji kama wa minara, majengo ya ofisi, maduka ya rejareja na maghala, ambayo hapo awali yalitambuliwa kama ukodishaji wa muda mfupi (Operating leases) katika 'IAS 17'. Deni la pango lilitambuliwa kwa thamani ya sasa ya malipo ya mikataba ya pango kwa kipindi kilichobaki kwenye mikataba, kwa kutumia viwango vya riba vya kampuni.

Kwa miezi kumi na miwili iliyoishia tarehe 31 Machi 2020, matumizi ya kanuni mpya ya 'IFRS 16', yalisababisha kupungua kwa gharama za uendeshaji kwa Shilingi bilioni 121.2 kutokana na kutotambua gharama za pango za uendeshaji; kuongezeka kwa gharama za uchakavu kwa Shilingi bilioni 84.9 kutokana na haki za matumizi katika mali zilizokodishwa katika muda ambao zitatumika na vilevile ongezeko la gharama za kifedha kwa Shilingi bilioni 67.0 kutokana na riba katika salio la madeni ya pango. Haya yote yamesababisha kupungua kwa faida kabla la tozo za kodi kwa kiasi cha Shilingi bilioni 30.7.

Gharama¹

Jumla ya gharama imepungua kwa 11.5% hadi Shilingi bilioni 657.8. Ukiacha athari za kutumia kanuni ya 'IFRS 16', jumla ya gharama imeongezeka kwa 4.8% hadi Shilingi bilioni 779.0. Ongezeko la gharama limejumisha Shilingi bilioni 21.0 zinazohusiana na gharama za utekezaji wa mwongozo wa usajili kwa alama za vidole na COVID-19². Ukiacha gharama hizi, jumla ya gharama iliongezeka kwa 2.0%, ikiwa ni matumizi madogo kutokana na gharama zilizo pungua kwenyesimu zilizopigwa kwenda mitandao mingine kutokana na kupunguzwa gharama inayotozwa kwa kila dakika (MTR), na vilevile mafanikio makubwa kutokana na programu yetu ya kupunguza matumizi, 'Fit for growth'. Kwa upande mwingine, matumizi yaliongezeka kutokana na ongezeko la gharama za uendeshaji wa mtandao kufuatia ongezeko la ukubwa wa mtandao kutokana na uwekezaji unaoendelea na pia marekebisho ya mfumuko wa bei katika mikataba iliyopo ya huduma.

EBITDA

'EBITDA' ni mapato kabla ya riba, kodi na gharama za uchakavu, ambayo yaliongezeka kwa 26.4% hadi Shilingi bilioni 364.8, huku wastani wa 'EBITDA' kwenye mapato (margin) ukiimarika kwa pointi 7.1 hadi 35.3%. Ukiacha athari za kutumia 'IFRS 16', 'EBITDA' ilipungua kwa 15.6% hadi Shilingi bilioni 243.6. Kupungua huko kulitokana na kupungua kwa kasi ya ongezeko la mapato katika nusu ya pili ya mwaka, na vilevile kuongezeka kwa jumla ya matumizi ikiwa ni pamoja na gharama za usajili wa simu kwa alama za vidole. Tukiweka kando gharama za usajili kwa alama za vidole na za COVID-19, 'EBITDA' ilipungua kwa 8.3%.

Gharama za uwekezaji

Tumewekeza Shilingi bilioni 154.6; ukiondoa mali za kukodi, ikiwa ni sawa na asilimia 15.0% ya mapato. Tumeendeleza lengo la kuimarisha mtandao wetu wa data na kupanua huduma za 4G nchini kote. Minara mipya 460 ya 4G imejengwa mwaka huu, ikiambatana na ongezeko la uwekezaji katika mkongo wa mawasiliano ili kuhakikisha kwamba wateja wetu wa data wanapata huduma nzuri wanapotumia mtandao wetu. Tumeongeza pia minara mipya 253 ya 3G na kufikia jumla ya minara 2 682 na kuendelea kuboresha mtandao wetu kwa kuongeza uwezo katika minara yetu ya 3G. Tumetumia Shilingi bilioni 5.3 kwa kununua vifaa vya usajili kwa alama za vidole ili kuongeza kasi ya usajili wa wateja.

1. Gharama mbali na gharama za uchakavu.

2. Gharama za usajili kwa alama za vidole za Shilingi bilioni 15.6, Shilingi bilioni 1.7 ni uchakavu wa vifaa vya usajili kwa alama za vidole na Shilingi bilioni 5.5 zinazohusiana na janga la kuenea kwa COVID-19 na gharama za masuala ya kisheria.

Muhtasari wa taarifa za pamoja za faida na hasara na mapato mengine

| Shilingi (milioni) | Zimekaguliwa 2020 ¹ | Zimekaguliwa 2019 | |
|--|-----------------------------------|----------------------|--|
| Mapato | 1 032 667 | 1 024 587 | Mapato yameongezeka kwa 0.8% hadi Shilingi bilioni 1 032.7, ikichochea na ongezeko la mapato ya matumizi ya wateja kutokana na ongezeko kubwa la 9.8% la wateja ikifidiwa na kupungua kwa wastani wa mapato kwa mteja (ARPU) kutokana na kufungia huduma kwa wateja milioni 2.9 ambao hawakukamilisha usajili kwa alama za vidole na vilevile shinikizo kubwa la ushindani wa bei. |
| Gharama za moja kwa moja | (321 693) | (303 306) | |
| Gharama za wafanyakazi | (57 671) | (59 368) | |
| Gharama za kujitangaza | (30 571) | (36 311) | |
| Gharama nyingine za uendeshaji | (247 885) | (344 086) | |
| Gharama za Uchakavu | (268 762) | (165 834) | |
| Gharama za madeni chechefu | (10 086) | (349) | |
| Faida ya uendeshaji | 95 999 | 115 333 | Jumla ya gharama imepungua kwa 11.5% hadi Shilingi bilioni 657.8. Ukiacha athari za kutumia kanuni ya 'IFRS 16', jumla ya gharama imeongezeka kwa 4.8% hadi Shilingi bilioni 779.0. Ongezeko katika gharama linajumuisha Shilingi bilioni 21.0 za utekelezaji wa mwongozo wa usajili kwa alama za vidole na ugonjwa wa COVID-19 ³ . Ukiacha gharama hizi, jumla ya gharama imeongezeka kwa 2.0%. |
| Mapato ya fedha | 50 465 | 38 475 | |
| Gharama za kifedha | (86 470) | (19 891) | |
| Mapato kutokana na mabadiliko ya viwango vya kubadili fedha za kigeni | 356 | 970 | |
| Faida kabla ya kodi | 60 350 | 134 887 | Uchakavu umeongezeka kwa 62.1%, kwa kuchochea na athari za kutumia kanuni ya 'IFRS 16'. Ukiacha athari za kutumia kanuni ya 'IFRS 16', uchakavu umeongezeka kwa 10.9% ukichochea na kuendelea kwetu kuwekeza kwenye mtandao. |
| Gharama za kodi ya mapato | (14 588) | (44 126) | |
| Faida kwa mwaka | 45 762 | 90 761 | Gharama za madeni chechefu katika mwaka huu zinahusisha kiasi kilichotengwa kwa ajili ya hasara tarajiwa za madeni chechefu tunayowadai wateja na washirika wetu kibiashara. Madeni ya biashara yanaripotiwa kiasi halisi kikipunguzwa na kiasi cha hasara tarajiwa cha madeni hayo kwa mujibu wa tathmini ya menejimenti juu ya uwezo wa wadeni kurejesha mikopo hiyo. Madeni yote hupimwa ili kutathmini uwezekano wake wa kutokulipwa. Gharama za kushuka kwa thamani ya uwekezaji kwenye kampuni yetu tanzu ya Shared Networks Tanzania Limited ('SNT'), iliyonunuliwa mnamo Julai 2016. |
| Mapato mengine | - | - | |
| Jumla ya mapato halisi kwa mwaka wa mapato, baada ya kutoa kodi² | 45 762 | 90 761 | Gharama za kodi ya shilingi bilioni 14.6 ni pungufu kwa 66.9% ukilinganisha na kodi ya mwaka jana (2019: Shs bilioni 44.1). Gharama ya kodi ya mwaka uliopita inajumuisha adhabu na fidia ambazo haziruhusiwi kupunguzwa kwa minajili ya kukokotoa kiasi cha kodi kwa mujibu wa sheria. Kwa mwaka huu, kodi imepungua kutokana na malimbikizo ya ziada ya kodi yaliyokuwepo (Deferred Tax asset) pamoja na kupunguzwa thamani kwa mali zitokanazo na kampuni tanzu ya Shared Network Tanzania Limited (SNT). |
| Mapato ya msingi na mchanganyiko kwa kwa kila hisa (TZS) | 16 644 | 15 532 | |

- Kampuni imeanza kutumia 'IFRS 16' kuanzia tarehe 1 Aprili 2019 kwa kutumia njia iliyorekebisha ya kurudi nyuma. Hivyo taarifa ya fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2020 yamezingatia IFRS 16 hali matokeo yam waka uliotangulia yamezingatia IAS 17. Rejlea Maelezo 4 ya Taarifa za Fedha za Mwaka kwa taarifa zaidi.
- Kodi zote zinawahusu wamiliki wa kampuni mama.
- Gharama za usajili kwa alama za vidole za Shilingi bilioni 15.6, Shilingi bilioni 1.7 ni uchakavu wa vifaa vya usajili kwa alama za vidole na Shilingi bilioni 5.5 zinazohusiana na janga la kuenea kwa COVID-19 na gharama za masuala ya kisheria.

Muhtasari wa taarifa za pamoja za hali ya kifedha

| Shilingi (milioni) | Zimekaguliwa 2020 | Zimekaguliwa 2019 | |
|---|----------------------|----------------------|--|
| Mali | | | |
| Mali za kudumu | 1 298 663 | 857 074 | |
| Mali na mitambo | 1 123 945 | 646 288 | ● Mali na mitambo iliongezekwa kwa 73.9% hadi Shilingi bilioni 1 123.9. Hii ni pamoja na mali kutokana na 'haki ya matumizi' zilizotambuliwa chini ya kanuni ya IFRS 16 ya Shilingi bilioni 505.6, ukiacha hii, mali na mitambo ilipungua kwa 4.6%. Uwekezaji uliofanyika katika mwaka huu ulifidiwa na uchakavu wa vifaa vya miundombinu ya mtandao kutoka uwekezaji wa miaka iliyopita. |
| Mali zisizoshikika | 78 510 | 74 740 | |
| Malipo ya Haki ya matumizi kabla ya kutumia | 54 888 | 58 385 | |
| Hasara iliyo ahirishwa | – | 48 593 | ● Hasara iliyoahirishwa inahusiana na mauzo na kukodisha baada ya mauzo, ya minara kwa Helios Towers, ambapo mapato yalikuwa madogo kuliko thamani iliyokadiriwa ya mali zilizouzwa. Katika miaka iliyotangulia, hasara hii iligawanywa kwa muda wa miaka 12 ya mkataba wa kukodisha. Kufuatia kutumia 'IFRS 16', uongozi umetathmini kuwa hasara iliyobaki iwe ni malipo ya awali ya pango. |
| Thamani isiyoshikika ya uwekezaji | 1 639 | 1 639 | |
| Kodi ya mapato inayotarajiwa kurejeshwa | 23 755 | 19 724 | |
| Madeni ya kibiashara na madeni mengine | 15 926 | 7 705 | |
| Mali za kudumu zilizotengwa kuuzwa | – | 1 307 | |
| Mali za muda mfupi | 1 097 226 | 1 134 121 | |
| Malipo ya Haki ya matumizi kabla ya kutumia | 13 657 | 11 527 | |
| Mali ghalani | 2 004 | 2 145 | |
| Madeni ya kibiashara na madeni mengine ya kulipwa | 100 815 | 126 232 | |
| Kodi ya mapato inayotarajiwa kurejeshwa | 4 723 | – | |
| Rasilimali za kifedha | 337 556 | 378 019 | |
| Uwekezaji wa muda mfupi | 164 643 | 219 576 | |
| Fedha taslimu na mbadala wa fedha | 473 828 | 396 622 | |
| Jumla ya mali | 2 395 889 | 1 992 502 | ● Ongezeko katika kodi iliyolipwa ziada limetokana na malipo yaliyolipwa kupinga makadirio ya kodi ya mwaka 2017 na 2018. |
| Mtaji na Madeni | | | |
| Mtaji na madeni | 1 255 152 | 1 263 844 | ● Amana za wateja wa M-Pesa ambazo haziwezi kutumika kwa matumizi mengine. |
| Mtaji wa hisa | 112 000 | 112 000 | |
| Malipo ziada kwenye hisa | 442 435 | 442 435 | |
| Mchango wa mtaji | 27 698 | 27 698 | |
| Ziada ya faida iliyotunzwa | 673 019 | 681 711 | |
| Madeni ya muda mrefu | 513 575 | 100 790 | ● Hali ya fedha taslimu imeongezeka kwa 19.5% hadi Shilingi bilioni 473.8 kutokana na kukomaa kwa hawala za serikali ambazo zilibadilishwa kutoka uwekezaji wa muda mfupi kuwa fedha taslimu, na vilevile ongezeko kutokana na mzunguko wa fedha katika biashara. |
| Madeni ya pango | 494 354 | 5 801 | |
| Ruzuku za serikali | 1 616 | 2 922 | |
| Kodi iliyoahirishwa | 13 800 | 45 687 | |
| Madeni ya kibiashara na madeni mengine ya kulipa | 186 | 46 380 | |
| Tahadhari ya madeni | 3 619 | – | |
| Madeni ya muda mfupi | 627 162 | 627 868 | ● Kufika tarehe 31 Machi 2020, uwekezaji wetu wa muda mfupi katika hawala za serikali ulikuwa Shilingi bilioni 164.6. |
| Madeni ya pango | 50 869 | – | |
| Madeni ya biashara na mengine ya kulipa | 552 167 | 584 018 | |
| Riba inayodaiwa na wateja wa M-Pesa | 11 992 | 31 577 | |
| Malipo ya kodi yanayodaiwa | – | 1 983 | |
| Ruzuku za serikali | 2 310 | 2 379 | |
| Tahadhari ya madeni | 9 824 | 7 911 | ● Madeni ya pango yanahusiana na kutambuliwa kwa madeni ya pango katika kutumia kanuni ya IFRS 16 ya Shilingi bilioni 545.2 ambapo Shilingi bilioni 50.9 zinakomaa ndani ya mwaka mmoja. |
| Jumla ya madeni | 1 140 737 | 728 658 | |
| Jumla ya mtaji na madeni | 2 395 889 | 1 992 502 | |

Muhtasari wa taarifa za pamoja za mzunguko wa fedha

| Shilingi (milioni) | Zimekaguliwa 2020 | Zimekaguliwa 2019 |
|--|----------------------|----------------------|
| Mzunguko wa fedha kutokana na shughuli za uendeshaji | | |
| Fedha zilizozalishwa kutokana na uendeshaji | 344 244 | 318 541 |
| Malipo ya kodi ya mapato | (53 181) | (45 198) |
| Mzunguko ghafi wa fedha kutokana na shughuli za uendeshaji | 291 063 | 273 343 |
| Mzunguko wa fedha zilizotumika katika shughuli za uwekezaji | | |
| Nyongeza katika mali na mitambo, na mali zisizoshikika | (159 350) | (184 843) |
| Mapato kutokana na mauzo ya mali na mitambo | 719 | 20 |
| Ruzuku za serikali zilizopokelewa | 2 838 | 2 489 |
| Marejesho ya uwekezaji wa muda mfupi | 54 933 | (89 307) |
| Mapato ya fedha yaliyopokelewa | 31 118 | 9 557 |
| Fedha zilizowekwa kwenye akiba za muda maalum | 40 463 | (25 143) |
| Riba kutoka amana za M-Pesa | 19 347 | 19 841 |
| Mzunguko halisi wa fedha katika shughuli za uwekezaji | (9 932) | (267 386) |
| Mzunguko wa fedha kutokana na shughuli za ugharimiaji | | |
| Magawio tulilolipa | (54 459) | (38 783) |
| Riba zilizolipwa kwa wateja wa M-Pesa | (39 013) | (11 107) |
| Riba iliyolipwa katika mikopo mingine | - | (324) |
| Riba ya madeni ya pango iliyolipwa | (67 034) | - |
| Malipo ya madeni ya pango – mtaji | (43 455) | - |
| Mzunguko halisi wa fedha zilizotumiwa katika shughuli za ugharimiaji | (203 961) | (50 214) |
| Ongezeko/(punguzo) ghafi katika fedha na fedha mbadala | 77 170 | (44 257) |
| Fedha taslimu na fedha mbadala tarehe 1 Aprili | 396 622 | 439 889 |
| Athari za mabadiliko ya viwango vya kubadili fedha katika fedha taslimu na fedha mbadala zilizo katika fedha za kigeni | 36 | 990 |
| Fedha taslimu na fedha mbadala kufika tarehe 31 Machi | 473 828 | 396 622 |

Kodi ya mapato iliongezeka kwa 17.7% kutokana na malipo ya kodi ya utangulizi yaliyofanyika kupinga makadirio ya kodi ya mwaka 2017 na 2018.


Hii inahusiana na uwekezaji wa Hawala za Serikali zilizokomaa mwishoni mwa mwaka.

Malipo ya pango ya Shilingi bilioni 110.5 yakijumuisha Shilingi bilioni 67.0 za riba ya pango na Shilingi bilioni 43.5 za deni la msingi wa pango zinazofuata masharti ya IFRS 16.

Viongozi wetu

Tuna Bodi yenye wakurugenzi 12, wengi wao ni wakurugenzi wasio watendaji. Mwenyekiti wetu ni mkurugenzi huru.

Muundo wa Bodi



1. Ali A. Mufuruki¹ (61)
Aliteuliwa mnamo Agosti 2017

- Uzoefu mkubwa wa uongozi
- Mtaalamu wa uongozi wa Mashirika
- Mahusiano na serikali

2. Hisham Hendi (40)
Aliteuliwa mnamo tarehe 19 Machi 2019

- Kiongozi mwerevu wa biashara
- Uzoefu wa masoko anuwai yanayoibukia
- Utekelezaji madhubuti wa ubunifu wa bidhaa na matoleo mapya

3. Jacques Marais (54)
Aliteuliwa mnamo Julai 2016

- Ujuzi wa kutosha wa masuala ya fedha
- Uzoefu mkubwa wa masoko yanayoibukia
- Ujuzi mkubwa wa masuala ya sekta ya mawasiliano ya simu

4. Andries Daniel Jan Delpoort² (56)
Aliteuliwa mnamo Aprili 2015

- Maarifa na uzoefu mkubwa katika teknolojia ya mawasiliano ya simu
- Utaalamu wa uongozi wa kimkakati
- Utaalamu wa uendeshaji na utekelezaji wa mikakati

5. Margaret Ikongo* (63)
Aliteuliwa mnamo Novemba 2017

- Utaalamu wa fedha
- Uhusiano na serikali
- Utaalamu wa uongozi wa Mashirika

6. Kenneth Kwame Gomado (42)
Aliteuliwa mnamo Machi 2018

- Uzoefu wa masoko anuwai yanayoibukia ya kifedha
- Ujuzi mkubwa wa sekta za mawasiliano ya simu na FMCG
- Uzoefu wa ushauri wa masuala ya Ukaguzi wa hesabu za fedha

7. Diego Gutierrez (45)
Aliteuliwa mnamo Machi 2018

- Mpanga mikakati ya kibiashara
- Maarifa mapana kuhusu teknolojia ya simu na uzoefu wa soko linaloibuka
- Utaalamu wa uongozi wa kimkakati

8. Matimba Mbungela (48)
Aliteuliwa mnamo Agosti 2017

- Maarifa na uzoefu mkubwa wa usimamizi wa vipaji
- Utaalamu katika taratibu bora za kushughulikia rasilimali watu
- Uzoefu wa uendeshaji wa shughuli za kimataifa

9. Winifred Ouko (50)
Aliteuliwa mnamo Novemba 2017

- Utaalamu wa fedha
- Uzoefu wa uendeshaji na utekelezaji wa mikakati kimataifa

10. Thembeke Semane (44)
Aliteuliwa mnamo Novemba 2017

- Utaalamu wa utawala wa Mashirika
- Uzoefu wa utekelezaji wa shughuli za uendeshaji na mikakati
- Utaalamu wa fedha

11. Henry JC Surtees³ (50)
Aliteuliwa mnamo Mei 2011

- Uzoefu wa masuala ya fedha
- Utaalamu wa utawala wa Mashirika
- Utaalamu wa uongozi wa Mashirika

12. Till Streichert⁴ (46)
Aliteuliwa mnamo Agosti 2017

- Uzoefu mbalimbali wa masuala ya fedha kimataifa
- Historia ya uongozi wa juu
- Umaizi wa sekta ya TEHAMA kimataifa

A Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji

R Kamati ya Ujira

N Kamati ya Uteuzi

* Ms. Margaret Ikongo amekuwa Mwenyekiti wa Muda tangu Desemba 2019.

Kumbuka:

- 1 Bw Ali A. Mufuruki alijiuzulu tarehe 1 Desemba 2019 na alifariki mnamo tarehe 7 Desemba 2019.
- 2 Bw Andries Daniel Jan Delpoort alijiuzulu tarehe 18 Mei 2020.
- 3 Bw Henry JC Surtees alijiuzulu tarehe 18 Machi 2020.
- 4 Bw Till Streichert alijiuzulu tarehe 30 Juni 2020.

Kamati ya Utendaji


Mkurugenzi Mtendaji



Fedha



Biashara: Wateja binafsi



Biashara: M-Pesa



Biashara: Wateja wa biashara




Mtandao



Sheria na Udhibiti



Masuala ya Shirika



Huduma kwa wateja



Rasilimali watu



TEHAMA



Huduma za Digitali



Dharura na Utekelezaji



1. Hisham Hendi (40)
Mkurugenzi Mkuu
Alijiunga Vodacom mwaka 2014,
Alijiunga Vodafone mwaka 2003

4. Epimack Mbeteni (42)
Mkurugenzi wa Biashara – M-Pesa
Alijiunga Vodacom mwaka 2014

7. Olaf Mumburi (44)
Mkurugenzi wa Sheria na Udhibiti
Alijiunga Vodacom mwaka 2008

10. Vivienne Penessis (45)
Mkurugenzi Rasilimali Watu
Alijiunga Vodacom mwaka 2018

2. Jacques Marais (54)
Mkurugenzi wa Fedha
Alijiunga Vodacom mwaka 2001

5. Arjun Dhillon (40)
Mkurugenzi wa Biashara – Wateja wa Kibiashara
Alijiunga Vodacom mwaka 2017,
Safaricom mwaka 2015

8. Rosalynn Gloria Mworira (40)
Mkurugenzi Masuala ya Mahusiano
Alijiunga Vodacom mwaka 2008

11. Luis Fedriani (48)
Mkurugenzi: TEHAMA
Alijiunga Vodacom mwaka 2012

3. Linda Riwa (33)
Mkurugenzi wa Biashara – Wateja Binafsi
Alijiunga Vodacom mwaka 2017

6. Andrew Lupembe (47)
Mkurugenzi Masuala ya Mtandao
Alijiunga Vodacom mwaka 2007

9. Harriet Atweza Lwakatare (42)
Mkurugenzi Huduma kwa Wateja
Alijiunga Vodacom mwaka 2012

12. Nguvu Kamando (45)
Mkurugenzi wa Huduma za Kidigitali
Alijiunga Vodacom mwaka 2002

13. Tax Agapinus (55)
Mkurugenzi Dharura na Utekelezaji
Alijiunga Vodacom mwaka 2020

Nguvukazi Yetu



Jumla ya wafanyakazi
551
(2019: 548)

Taarifa ya uongozi wa shirika



Taarifa ya utekelezaji

Vodacom Tanzania Public Limited Company ('Vodacom Tanzania') inajizatiti kutoa huduma zenye ubora wa hali ya juu kwa uaminifu, maadili na utaalamu katika biashara.

Kanuni za uongozi wa kampuni zinajumuisha nidhamu, uhuru, uwajibikaji, usawa, uwajibikaji kwa jamii, uwazi na uwajibikaji wa wakurugenzi kwa wadau. Kanuni hizi zinazingatiwa katika taratibu za udhibiti wa ndani na sera za Vodacom Tanzania zinazoongoza utendaji wa kampuni na zinawiana na miongozo ya Soko la Hisa na Mtaji na Dhamana kuhusu taratibu za usimamizi wa shirika unaofanywa na kampuni za umma zilizoorodheshwa nchini Tanzania.

Muundo wa usimamizi wa shirika

Mchoro ufuatao unaonesha muundo wa uongozi wa Vodacom Tanzania tarehe 31 Machi 2020:



Maadili ya viongozi

Bodi inakubali uwajibikaji wa pamoja katika kueleza namna ambavyo maadili na tabia za kimaadili zinapaswa kutekelezwa katika Vodacom Tanzania. Hii ni pamoja na kupanga taratibu za utendaji wa wajumbe wa Bodi ili kuhakikisha kuwa wanatenda kwa uadilifu, uzoefu, uwajibikaji, haki na uwazi. Sifa hizi zinazingatia maoni kuanzia juu kuzinagtia maadili ndani ya Vodacom Tanzania.

Uongozi na Kamati za Bodi

Bodi

Vodacom Tanzania ina Bodi yenye wakurugenzi 12, ambapo kati yao wanne (pamoja na Mwenyekiti) ni wakurugenzi huru wasio watendaji, sita kati yao si watendaji (lakini si huru kwa kuwa wanawakilisha wadau wakuu), na wawili ni wakurugenzi watendaji.

Bodi imeridhika kuwa uwiano wa wataalamu wenye maarifa, ujuzi na uzoefu wa aina mbalimbali ni wa kutosha katika Bodi. Bodi inaweza kukutana kwa ajili ya kufanya shughuli, kuahirisha na vinginevyo kudhibiti mikutano yake itakavyoona inafaa. Mikutano ya Bodi inafanyika mara kwa mara kupitia mkakati, ufanisi wa kiuendeshaji na kifedha, na vilevile kusimamia. Mikutano Maalum ya Bodi inaweza kufanyika wakati itakapohitajika. Kamati ya Ujira na Uteuzi hupitia mara kwa mara utaratibu wa Bodi na kamati kupokezana madaraka ili kuhakikisha tunakuwa na watu sahihi wenye ujuzi na uzoefu kwa siku zijazo. Mkurugenzi Mkuu ana wajibu wa kuhakikisha kuwa viongozi muhimu wana ujuzi, mamlaka na rasilimali za kutosha kutekeleza mkakati wa Vodacom Tanzania.

Uwajibikaji

Bodi ina wajibu wa kuhakikisha Vodacom Tanzania inakuwa na mafanikio. Kazi yake ni kuongoza na kutoa uamuzi wa busara katika kuelekeza Vodacom Tanzania kufanikisha ukuaji endelevu na kutenda kwa maslahi ya wadau wake. Kwa mujibu wa utendaji bora, kazi za Mwenyekiti na Mkurugenzi Mkuu ni tofauti. Mwenyekiti anawajibika kuongoza Bodi, wakati Mkurugenzi Mkuu anawajibika kusimamia uendeshaji wa Vodacom Tanzania.

Katiba ya Bodi inaeleza wajibu wa Bodi, ambao ni pamoja na:

- Kufanya uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu na Mkurugenzi wa Fedha;
- Kusimamia kwa karibu mwelekeo wa kimkakati wa Vodacom Tanzania;
- Kupitisha miradi mikubwa, ununuzi au mauzo ya vitu;
- Kufanya uamuzi wa busara kuhusu masuala ya biashara ya Vodacom Tanzania, mbali na menejimenti;
- Kuhakikisha kuwa miundo, sera na taratibu stahiki zinakuwepo;
- Kuhakikisha udhibiti wa ndani wa Vodacom Tanzania unakuwa na mafanikio;
- Kupitia na kutathmini dharura za Vodacom Tanzania;
- Kupitisha bajeti ya mwaka na mpango wa utekelezaji;
- Kupitisha matokeo ya pamoja fedha ya mwaka na ya muda na vilevile mawasiliano kwenda kwa wadau;
- Kupitisha muundo wa viongozi waandamizi, wajibu na mipango ya kupokezana madaraka; na
- Usimamizi wa habari na teknolojia.

Wakurugenzi

Katiba ya Vodacom Tanzania inaeleza kuwa wakurugenzi wote watastaafu kwa zamu na kustahili kuchaguliwa tena na wadau angalau mara moja katika kila miaka mitatu.

Mwenyekiti

Katiba inaitaka Bodi kumchagua Mwenyekiti kila mwaka. Bodi inaridhika kuwa Mwenyekiti anaweza kufanya kazi zake za ofisi hii ipasavyo. Bi Margaret Ikongo aliteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Muda kuanzia tarehe 1 Desemba 2019 kufuatia kujiuzulu kwa marehemu Ali A Mufuruki. Aliteuliwa kushika nafasi hiyo hadi wakati utafutaji wa mtu wa kuchukua nafasi hiyo ya Mwenyekiti huru asiye mtendaji itakapokuwa imekamilika.

Kupata ushauri huru

Bodi inatambua kuwa inawezekana kukawa na wakati ambapo wakurugenzi wakaona kuwa ni muhimu kupokea ushauri huru wa kitaalamu. Kwa kawaida kulingana na utaratibu uliopo Vodacom Tanzania hugharimia shughuli hii.

Shughuli za uongozi wa shirika

Mikutano ya Bodi

Bodi hufanya mikutano isiyopungua minne kila mwaka, kukiwa na mikutano maalum ya Bodi inayoitishwa inapobidi. Mikutano nane maalum ya bodi ilifanyika mwaka huu.

Jedwali hapo chini linaonesha mahudhurio ya wakurugenzi katika mikutano ya Bodi kwa mwaka huu.

| Jina la Mkurugenzi | 6 Apr 2019 Maalum | 2 Mei 2019 Maalum | 23 Mei 2019 | 30 Mei 2019 | 17 Jul 2019 Maalum | 22 Agosti 2019 | 7 Okt 2019 Maalum | 15 Okt 2019 Maalum | 4 Nov 2019 Maalum | 5 Nov 2019 | 23 Jan 2020 Maalum | 19 Machi 2020 |
|--------------------------------|----------------------|----------------------|-------------|-------------|-----------------------|----------------|----------------------|-----------------------|----------------------|------------|-----------------------|---------------|
| Bw Ali A Mufuruki (Mwenyekiti) | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | R | R |
| Bw Till Streichert | ✓ | | X | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bw Matimba Mbungela | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bw Andries Delpport | ✓ | ✓ | X | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bw Henry Surtees | X | ✓ | X | X | ✓ | ✓ | X | X | ✓ | ✓ | ✓ | R |
| Bw Jacques Marais | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bw Hisham Hendi | X | X | X | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bi Margaret Ikongo | ✓ | ✓ | X | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | X | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bi Thembeke Semane | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | X | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bi Winifred Ouko | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bw Diego Gutierrez | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | X | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | X | ✓ |
| Bw Kenneth Gomado | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | X | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |

Zingatia:

1. Ali A Mufuruki alijiuzulu mnamo tarehe 1 Desemba 2019.
2. Henry Surtees alistaafu mnamo tarehe 10 Machi 2020.



Kamati za Bodi

Wakurugenzi wasio watendaji wanachangia uzoefu na maarifa waliyo nayo katika kamati za bodi. Kamati zote zinafanya kazi kwa kuzingatia katiba iliyopitishwa na Bodi, ambayo huboreshwa mara kwa mara kuendana na maendeleo katika sheria ya mashirika na taratibu bora za utendaji.

Bodi ina Kamati ya Ujira, Kamati ya Uteuzi na Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji, ambazo zinatekeleza shughuli maalum zilizopewa.

Kamati za Bodi zina wajibu wa kupitia na kusimamia shughuli kulingana na hadidi za rejea. Kila kamati inapaswa kuwa na wajumbe wa Bodi wasiopungua watatu au kama Bodi itakavyoona inafaa, alimradi kwamba kamati ifuate kanuni itakazokuwa imewekewa na Bodi na kwamba wajumbe wote wawe wajumbe wa kamati yoyote iliyoanzishwa.

Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji *

Wajumbe wa kamati: Margaret Ikongo (Mwenyekiti), Thembeka Semane na Winifred Ouko.

Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji ilianzishwa kwa kuzingatia utaratibu bora katika uongozi wa shirika. Kamati hii inaundwa na wakurugenzi watatu wasio watendaji. Mkurugenzi Mkuu na Mkurugenzi wa Fedha, na vilevile wakaguzi kutoka nje, wanahudhuria mikutano ya Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji kwa mwiliko.

Kazi ya msingi ya Kamati hii ni kuhakikisha kunakuwa na uaminifu katika kutoa ripoti ya fedha na mchakato wa ukaguzi na kuwa kunakuwepo mfumo thabiti wa usimamizi wa dharura na udhibiti wa ndani. Katika kutekeleza malengo haya, Kamati hii inasimamia mahusiano na wakaguzi wa nje na kupitia ufanisi wa ukaguzi wa ndani.

Wakaguzi wa ndani na nje wanaweza kumwona bila kikwazo Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji. Idara ya ukaguzi wa ndani huripoti moja kwa moja katika Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji na pia inawajibika kwa Mkurugenzi wa Fedha katika masuala ya siku hadi siku.

Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji inawajibika kufanya yafuatayo:

- Kupitia matokeo ya muda ya pamoja, matokeo ya awali, taarifa za fedha za mwaka za Vodacom Tanzania na kampuni zake tanzu (pamoja 'Kampuni');

- Kufuatilia utekelezaji wa sheria zilizopo na Kanuni za Soko la Hisa na Mtaji na Hisa la Dar es Salaam;
- Kuripoti kwenye Bodi kuhusu ubora na kukubalika kwa sera za uhasibu na taratibu za Kampuni, pamoja na sera na taratibu muhimu za hesabu;
- Kufanya usimamizi wa mchakato wa kutoa ripoti ya mwaka;
- Kufikiria uteuzi na/au kuwasimamisha wakaguzi wa nje, ikiwa ni pamoja na ada za ukaguzi wao, uhuru na bila upendeleo na kuamua aina na kiwango cha huduma zisizo za ukaguzi;
- Kupitisha mpango wa mwaka wa ukaguzi;
- Kupokea na kushughulikia ipasavyo malalamiko, ndani na nje yanayohusiana na taratibu za uhasibu na ukaguzi wa ndani au maudhui au ukaguzi wa vyombo vyote ndani ya taarifa za fedha za mwaka za Kampuni au mambo kama hayo;
- Kupitia na kufuatilia usimamizi na kuripoti mambo yote yanayohusiana na kodi;
- Kufuatilia kazi na michakato ya usimamizi wa dharura na kutathmini dharura kubwa zaidi za Kampuni; na
- Kufuatilia ufanisi wa michakato ya kujenga ufahamu na kujenga uelewa wa sheria husika ili kuhakikisha menejimenti inafanya utekelezaji.

Mikutano ya Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji isiyopungua mitatu imepangwa kufanyika katika kila mwaka wa fedha. Mikutano ya ziada ya kamati inaweza kuitishwa inapobidi. Mikutano mitano maalum ilifanyika katika mwaka huo.

Jedwali hapo chini linaonesha mahudhuro ya wakurugenzi katika mikutano ya Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji kwa mwaka huo.

| Jina la Mkurugenzi | 2 Mei 2019 Maalum | 9 Mei 2019 Maalum | 30 Mei 2019 | 17 Jul 2019 Maalum | 22 Agost 2019 | 4 Nov 2019 Maalum | 5 Nov 2019 | 23 Jan 2020 Maalum | 19 Machi 2020 |
|--------------------|----------------------|----------------------|-------------|-----------------------|---------------|----------------------|------------|-----------------------|---------------|
| Bi Margaret Ikongo | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bi Thembeka Semane | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bi Winifred Ouko | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |

* Winifred Ouko amekuwa akifanya kazi kama Mwenyekiti wa Muda tangu Desemba 2019.

Shughuli za uongozi wa shirika

inaendelea

Kamati ya Ujira

Wajumbe wa kamati: Winifred Ouko (Mwenyekiti), Diego Gutierrez na Matimba Mbungela.

Kamati ya Ujira inafanya kazi ya kuwezesha na kusaidia Bodi kutekeleza wajibu wake kwa:

- Kuamua na kukubaliana kuhusu ujira na kifurushi kizima cha mafao kwa viongozi, isipokuwa wafanyakazi walioazimwa;
- Kuamua, kukubaliana na kuandaa sera ya jumla ya ujira ya Vodacom Tanzania na kuhakikisha kuwa inalingana na sera ya ujira ya Vodacom Group Limited;

- Kuhakikisha kuwa mikakati na programu za ujira zenye kuzingatia haki na ushindani zinakuwepo ili kuwezesha kuajiri, kutoa motisha na kuwabakiza wafanyakazi wenye ufanisi mkubwa katika ngazi zote kusaidia kufanikisha malengo ya kampuni na kulinda maslahi ya wadau;
- Kupitia na kupendekeza kwa Bodi vigezo muhimu vya kupima ufanisi wa viongozi watendaji katika kutekeleza kazi na majukumu yao;
- Kuandaa na kutekeleza sera ya falsafa ya ujira;
- Kuzingatia maslahi au mipango mingine maalum ya kifedha;
- Kuhakikisha utekelezaji wa sheria na kanuni zinazohusika.

Jedwali hapo chini linaonesha mahudhurio ya wakurugenzi katika mikutano ya Kamati ya Ujira mwaka huu.

| Jina la mkurugenzi | 30 Mei 2019 | 17 Jul 2019 Maalum | 22 Agosti 2019 | 5 Sept 2019 | 5 Nov 2019 | 19 Machi 2020 |
|---------------------|-------------|-----------------------|----------------|-------------|------------|---------------|
| Bi Winifred Ouko | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bw D Gutierrez | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | X |
| Bw Henry Surtees | ✓ | ✓ | X | X | ✓ | R |
| Bw Matimba Mbungela | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |

Zingatia:

1. Henry Surtees alistaafu tarehe 10 Machi 2020.

Kamati ya Uteuzi

Wajumbe wa kamati: Margaret Ikongo (Mwenyekiti wa Muda), Winifred Ouko na Matimba Mbungela.

Kamati ya Uteuzi inafanya kazi kuwezesha na kusaidia Bodi kutekeleza majukumu yake kwa:

- Kufuatilia ukubwa na wajumbe wanaounda Bodi;
- Kupendekeza watu kwa ajili ya uteuzi kama wajumbe wa Bodi na kamati zake;
- Kupitia mipango ya kupokezana madaraka;

- Kuhakikisha kuwa ufanisi wa wajumbe wa Bodi unapitiwa;
- Kuamua mchanganyiko na ufanisi wa bodi za kampuni tanzu za Vodacom Tanzania;
- Kupitisha uteuzi wa watu katika bodi husika za kampuni tanzu za Vodacom Tanzania;
- Kuhakikisha kustahili kwa wajumbe wa Bodi katika nafasi zao;
- Kupitia muundo wa shirika kuhakikisha kuwa unakidhi haja, kutekeleza mkakati na malengo ya muda mrefu ya kibiashara; na
- Kuhakikisha utekelezaji wa sheria na kanuni husika.

Jedwali hapo chini linaonesha mahudhurio ya wakurugenzi kwenye mikutano ya Kamati ya Uteuzi mwaka huu.

| Jina la mkurugenzi | 25 Apr 2019 Maalum | 30 Mei 2019 | 17 Jul 2019 Maalum | 7 Agosti 2019 Maalum | 22 Agosti 2019 | 4 Nov 2019 | 17 Machi 2020 |
|---------------------|-----------------------|-------------|-----------------------|-------------------------|----------------|------------|---------------|
| Bi Winifred Ouko | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bw Ali A Mufuruki | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | R |
| Bw Matimba Mbungela | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bi Margaret Ikongo | | | | | | | ✓ |

Zingatia:

1. Ali A. Mufuruki alijiuzulu tarehe 1 Desemba 2019.

Mikutano ya Bodi za Kampuni Tanzu za Vodacom Tanzania PLC

Jedwali lifuatalo linaonesha mahudhurio ya wakurugenzi katika mikutano ya Bodi ya Shared Networks Tanzania Limited mwaka huu.

| Jina la mkurugenzi | 29 Mei 2019 | 21 Agosti 2019 | 4 Nov 2019 | 18 Machi 2020 |
|--------------------|-------------|----------------|------------|---------------|
| Bw Jacques Marais | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bw Alec Mulonga | ✓ | ✓ | ✓ | R |
| Bw Olaf Mumburi | | | | ✓ |

Zingatia:

- Alec Mulonga alistaafu tarehe 1 Januari 2020.
- Olaf Mumburi aliteuliwa tarehe 18 Machi 2020.

Jedwali lifuatalo linaonesha mahudhurio ya wakurugenzi kwenye mikutano ya Bodi ya Vodacom Trust Limited mwaka huu.

| Jina la mkurugenzi | 29 Mei 2019 | 21 Agosti 2019 | 4 Nov 2019 | 18 Machi 2020 |
|--------------------|-------------|----------------|------------|---------------|
| Bw Jacques Marais | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bw Kenneth Gomado | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |

Jedwali lifuatalo linaonesha mahudhurio ya wakurugenzi kwenye mikutano ya Bodi ya M-Pesa Limited mwaka huu.

| Jina la mkurugenzi | 29 Mei 2019 | 21 Agosti 2019 | 4 Nov 2019 | 18 Machi 2020 |
|---------------------------|-------------|----------------|------------|---------------|
| Bw Jacques Marais | | | ✓ | ✓ |
| Bw Sitoyo Lopokoiyit | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bw Christopher Williamson | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bw Olaf Mumburi | | | | ✓ |
| Bw Evans Lyimo | ✓ | ✓ | R | R |
| Bw Epimack Mbeteni | | | ✓ | ✓ |
| Bw Hisham Hendi | | | ✓ | R |

Maelezo:

- Epimack Mbeteni, Jacques Marais, Hisham Hendi na Olaf Mumburi waliteuliwa tarehe 4 Novemba 2019.
- Evans Lyimo alistaafu tarehe 4 Novemba 2019.
- Hisham Hendi alistaafu tarehe 18 Machi 2020.

Jedwali lifuatalo linaonesha mahudhurio ya wakurugenzi kwenye mikutano ya Bodi ya Vodacom Tanzania Foundation mwaka huu.

| Jina la mkurugenzi | 29 Mei 2019 | 21 Agosti 2019 |
|----------------------|-------------|----------------|
| Bw Jacques Marais | ✓ | ✓ |
| Bi Taki Netshitenzhe | X | ✓ |
| Bi Rosalynn Mworira | ✓ | ✓ |

Maelezo:

- Vodacom Tanzania Foundation ilifutwa kwenye orodha ya makampuni kuanzia tarehe 31 Agosti 2019 kulingana na Sheria Namba 3 ya mwaka 2019 yenye Marekebisho madogo madogo.



Taarifa ya Masuala ya Ujira

Taarifa hii inatoa muhtasari wa falsafa na sera ya ujira ya Vodacom Tanzania kwa wakurugenzi watendaji na wasio watendaji. Pia inatoa ufafanuzi wa namna sera ilivyotekelezwa.

Barua kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ujira:

Wapendwa Wanahisa

Sehemu ya shabaha yetu ni kusaidia na kuishauri Bodi kuhusu masuala yanayohusiana na ujira wa wakurugenzi watendaji. Tunahakikisha kuwa falsafa na sera ya ujira inasaidia Malengo ya kimkakati ya Kampuni kuwezesha kuajiri, kutoa motisha na kubakiza watendaji, kwa lengo la kuongeza thamani ya wanahisa na kutekeleza sheria na miongozo iliyotolewa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ('CMSA').

Kamati imezingatia matakwa ya kutoa taarifa ya Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, ya mwaka 1994 na imetoa taarifa ifuatayo, ambayo inafuata miongozo kuhusu taratibu za uendeshaji wa kampuni zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa nchini Tanzania wakati tukielewa kuhusu utoaji wa taarifa nyeti za mtu au soko. Ninapenda kutoa shukrani kwa wajumbe wenzangu wa kamati kwa kuendelea kuniunga mkono, na ninataraji kuendelea kufanya kazi nao mwaka ujao.

Winifred Ouko

Mwenyekiti wa Kamati ya Ujira



Kulingana na miongozo ya CMSA kuhusu taratibu za udhibiti wa makampuni yaliyoorodheshwa kwenye Soko la Hisa nchini Tanzania, taarifa hii inaeleza sera za Vodacom Tanzania za ujira kwa wakurugenzi watendaji na wakurugenzi wasio watendaji hususan kiasi na aina za ujira kwa wakurugenzi ikiwa ni pamoja na wakurugenzi wasio watendaji kwa pamoja.

Falsafa, sera na mfumo wetu wa ujira kwa mwaka huu ni kwa wakurugenzi watendaji.

Lengo letu ni kuwavutia, kubaki nao na kuwapatia motisha watendaji wenye uwezo wa hali ya juu, sambamba na kulinganisha ujira wao na maslahi ya wanahisa na taratibu bora za utekelezaji. Utaratibu wetu ni kutoa ujira wa jumla, linganifu wenye vipengele vifuatavyo:

- ▶ Ujira hakika (GP);
- ▶ Motisha ya muda mfupi (STIP);
- ▶ Motisha ya muda mrefu (LTIP);
- ▶ Programu mbalimbali za utambuzi;
- ▶ Fursa mbalimbali za kujifunza na kujiendeleza;
- ▶ Mazingira ya kazi ya yanayovutia; na
- ▶ Programu nzuri ya ustawi wa wafanyakazi.

Viongozi watendaji wanafuata falsafa ya 'Jumla ya gharama kwa kampuni', ambayo tunairejelea kama ujira uhakika (GP). Michango katika huduma za tiba, fedha za ustaafu na mafao ya bima yamejumuishwa katika GP.

Vipengele hivyo hapo juu vinaendana na kuimarishwa na utaratibu wetu wa kutatmini utendaji kazi na (PD) na kusimamia vipaji. Sera yetu ni kuwapa marupurupu viongozi wetu watendaji kutokana na michango yao katika ufanisi wetu kimkakati, kifedha na kiutendaji. Ili kuwa muajiri anayeheshimika katika sekta yetu tunahitaji kuvutia, kuendelea na kubakiza vipaji bora na rasilimali ya wataalamu wa ndani na kimataifa.

Kila mwaka tunalinganisha viwango na kuongeza malipo katika GP kulingana na soko, ufanisi binafsi na uwezo. Tathmini ya ufanisi binafsi na uwezo wa kiutendaji hubainishwa kupitia utaratibu wetu wa kupima utendaji na uwezo wa kiutendaji wa wafanyakazi wetu. Matokeo ya utaratibu huu, huchangia katika uamuzi wa mabadiliko ya motisha ya muda mfupi na muda mrefu.

Kila mwaka, tunaendesha zoezi la kulinganisha ujira wa wafanyakazi na wafanyakazi wengine wa aina yao katika soko kulingana na ufanisi na uwezo binafsi wa kila mfanyakazi ambayo huchangia ongezeko la GP.

Motisha yetu ya muda mfupi inayolipwa kama bonasi ya fedha taslimu hutokana na kiwango cha kufikiwa malengo kwenye utendaji wa mambo ya fedha, mikakati, uendeshaji wa vitengo na malengo binafsi ambayo kila mtendaji amepewa. Kiasi kilichopo kwa ajili ya motisha ya muda mfupi kinatokana na utendaji kwenye mambo ya fedha kadiri ya malengo yaliyowekwa na kukubaliwa.

Viongozi watendaji ambao wametumwa Vodacom Tanzania kutoka Vodacom Group Limited, hulipwa motisha ya muda mrefu kulingana na taratibu za kundi la makampuni la Vodacom Group, ambapo hupewa umiliki wa hisa na mwajiri wao. Hii huchochea utendaji unao akisi umiliki na uaminifu, na huchangia katika lengo la Vodacom kuwabakisha watendaji hodari.

Mfumo huo ni mfumo kamili wa umiliki, na matokeo yake wahusika hupata gawio kutoka siku walipopewa hisa japokuwa thamani ya hisa inaweza tu kupatikana baada ya miaka mitatu na ni kwa kulingana na kiwango ambacho masharti ya kupewa hisa hizo yametimizwa.

Utoaji taarifa za ujira wa wakurugenzi watendaji na wasio watendaji

Ujira wa Wakurugenzi watendaji

Ujira wa wakurugenzi watendaji ulifanyiwa marejeo kwa kuzingatia ulinganifu na ujira wa watendaji wengine katika soko, na pia athari za kushindwa kuwabakiza watendaji muhimu katika menejimenti.

Taarifa za ujira wa wakurugenzi watendaji na wasio watendaji zipo katika Maelezo 38 (pande husika) za taarifa za pamoja za mwaka za fedha katika ukurasa namba 119 mpaka 120 wa taarifa hii ya mwaka.

Kutekeleza Sera

Kwa kuzingatia utaratibu/sera ya ujira, taarifa iliyo kwenye toleo hili ni kwa wafanyakazi waliostahili, ambapo maamuzi yote yahusuyo ujira yamefanywa kwa kuzingatia utaratibu wa ujira kama ulivyopitishwa. Kama ilivyo kwa mwaka uliotanguliwa, hakuna mabadiliko yaliyofanywa katika utekelezaji wa sera/utaratibu wa ujira katika mwaka huu.



*Vigezo & Masharti kuzingatwa.

SMART
KITOCHI

Pic to be replaced

4G

24GB
DAKIKA 600
& SMS 3000

BURE KWA
MIEZI 6

Yako!
Kutoka
kwetu



Pata Smart Kitochi kutoka maduka ya Vodacom nchi nzima kwa **Tsh 48,000** tu.

Yajayo yanafurahisha.
Uko tayari?

 **vodacom**

Maelezo ya hesabu za fedha za mwaka

kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2020

Yaliyomo

28

Taarifa ya wakurugenzi

35

Tamko la majukumu ya wakurugenzi

35

Tamko la Mkuu wa kitengo cha fedha

36

Taarifa ya Mkutano Mkuu wa Mwaka

41

Fomu ya Mwakilishi

43

Taarifa kuhusu umiliki

43

Taarifa za Kampuni

44

Dai la Haki

Taarifa ya wakurugenzi

Kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2020

Wakurugenzi wanawasilisha taarifa yao pamoja na taarifa iliyokaguliwa ya jumla ya fedha ya Vodacom Tanzania Public Limited Company ('Kampuni'), na kampuni zake tanzu (kwa pamoja, 'Kundi Kampuni') kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2020.

Aina ya biashara

Kundi la Kampuni huendesha biashara ya kutoa huduma ya mtandao wa mawasiliano ya simu na huduma za fedha kwa njia ya simu nchini Tanzania. Pia linatoa huduma nyingine za mawasiliano, ikiwa ni pamoja na huduma za mawasiliano ya kuunganishwa kwa waya.

Tathmini ya Masuala ya Kiuendeshaji na Kifedha

Matokeo kwa mwaka huu yamewekwa katika taarifa za pamoja na taarifa binafsi za faida au hasara na mapato mengine.

Mapato ya Kundi la Kampuni kwa mwaka yaliongezeka kwa 0.8% hadi Shilingi milioni 1 032 667 (2019: Shilingi milioni 1 024 587). Faida ya uendeshaji ya Kundi la Kampuni ilipungua kwa 16.8% hadi Shilingi milioni 95 999 (2019: Shilingi milioni 115 333). Faida halisi ya Kundi la Kampuni kwa mwaka ilipungua kwa 49.6%¹ hadi Shilingi milioni 45 762 (2019: Shilingi milioni 90 761).

Mapato ya Kundi la Kampuni kabla ya riba; kodi; uchakavu; ulipaji madeni; faida au hasara katika kuondosha mali, mitambo na mali zisizoshikika; na gharama zinazohusiana na malipo kwa kutumia hisa ('EBITDA') yaliongezeka kwa 26.5% hadi Shilingi milioni 364 996 (2019: Shilingi milioni 288 656) na kiwango cha EBITDA cha 35.4%, ikiwa ni ongezeko la alama 7.2 ukifananiwa na mwaka uliotangulia.

Wateja walio tumia huduma zetu katika kipindi cha siku 90 zilizopita wameongezeka hadi kufikia 15 513 000 (2019: 14 133 000) ikiwa ni ongezeko la 9.8% kwa mwaka (2019: 9.6%).

Gawio

Katika Mkutano Mkuu wa Mwaka ('AGM') uliofanyika tarehe 20 Septemba 2019, wanahisa walipitisha gawio la mwisho la jumla la Shilingi 20.43 (2019: Shilingi 17.33) kwa kila hisa, sawa na Shilingi milioni 54 454 (2019: Shilingi milioni 38 819), zilizolipwa kutoka katika akiba ya mapato ya mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Machi 2019.

Kiasi hicho cha gawio kilikuwa sawa na 60% (2019: 60%) ya faida halisi baada ya kodi.

Gawio la Shilingi milioni 54 454 zililipwa tarehe 18 Oktoba 2019 kwa wanahisa waliorekodiwa katika rejesta wakati wa kufunga biashara tarehe 22 Agosti 2019.

Bodi ya Wakurugenzi ('Bodi') itapendekeza gawio kwa ajili ya kupitishwa na wanahisa katika Mkutano Mkuu wa Mwaka kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Machi 2020 kulingana na sera ifuatayo ya gawio:

- Kampuni inakusudia kulipa sehemu kubwa ya faida yake baada ya kodi kadri itakavyopatikana baada ya kubakiza kiasi hicho na kulipa madeni kama itakavyokuwa muhimu kukidhi matakwa ya bajeti na mpango wa biashara, na kuzingatia fedha zinazotakiwa kwa ajili ya uwekezaji. Hakuna tarehe maalum iliyopangwa ya kustahili kupata gawio na tarehe ya malipo itapendekezwa na Bodi na kupitishwa na wanahisa wakati wa kutoa tamko, kwa kuzingatia matakwa ya taratibu za kuorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam ('DSE').

Kwa kuzingatia yaliyosemwa hapo juu, sera ya gawio ni kulipa angalau 50% ya faida baada ya kodi.

Uwezo wa kulipa madeni na ukwasi wa kampuni

Bodi inaona kuwa Kampuni ina uwezo wa kulipa madeni, kulingana na matakwa ya Sheria ya Makampuni, Na 12 ya mwaka 2002 ya Tanzania. Kampuni ilikuwa na mali za thamani ya Shilingi milioni 470 064 kwa 31 Machi 2020 (2019: mali zilikuwa za thamani ya Shilingi milioni 506 253) ambazo ni pamoja na fedha taslimu na uwekezaji wa Hawala za Serikali ya Tanzania jumla ya Shilingi milioni 638 471 (2019: Shilingi milioni 616 198).

¹ Kampuni ilianza kutumia kanuni ya uandaaji na uwasilishaji wa taarifa za Gharama za kukodi, 'IFRS 16' mnamo tarehe 1 Aprili 2019, hivyo taarifa ya fedha kwa mwaka unaoishia tarehe 31 Machi 2020 zimefuata utaratibu wa IFRS 16 wakati taarifa ambatanishwa ya mwaka 2019 inafuata kanuni ya awali ya 'IAS 17'. Athari kifedha za kuanza kutumia kanuni ya IFRS 16 zimeelezwa katika maelezo 4 ya taarifa za fedha za Kampuni.

Muundo wa mtaji na umiliki wa hisa

Umiliki wa hisa² zilizolipwa kwa asilimia kama inavyooneshwa hapo chini:

| | 2020 % | 2019 % |
|-----------------------|---------------|---------------|
| Vodacom Group Limited | 75.00 | 48.75 |
| Mirambo Limited | – | 26.25 |
| Wanahisa wengine | 25.00 | 25.00 |
| | 100.00 | 100.00 |

Mwaka huu, Vodacom Group Limited ilinunua 26.25% ya hisa zilikuwa zinamilikiwa na kampuni ya Mirambo.

Kundi la Kampuni linamilikiwa na kampuni mama, Vodacom Group Limited, ambayo mnamo tarehe 31 Machi 2020 ilikuwa inamiliki 75% ya hisa zinazomilikiwa moja kwa moja (31 Machi 2019: ilikuwa inamiliki 48.75% za hisa za Kampuni moja kwa moja, na 12.86% kupitia kampuni ya Mirambo ambayo ilikuwa inamiliki 26.25% za hisa za Kampuni), na kiasi kilichobaki 25% zikimilikiwa na umma.

Tarehe 31 Machi 2020, mtaji wa hisa ulioidhinishwa wa Kampuni la Kampuni ulikuwa Shilingi milioni 200 000 ikiwa ni hisa milioni 4 000 za kawaida zenye thamani ya Shilingi 50 kwa kila hisa, wakati mtaji wa hisa uliolipwa ni Shilingi milioni 112 000 unaotokana na hisa za kawaida 2 240 000 300 zenye thamani ya Shilingi 50 kwa kila hisa. Hakukuwa na mabadiliko katika mtaji wa hisa ulioidhinishwa na mtaji uliotolewa mwaka huu.

Gharama za uwekezaji

Mwaka huu, Kundi la Kampuni liliwekeza kiasi cha Shilingi milioni 159 393 (2019: Shilingi milioni 171 432³ mbali na kiasi cha shilingi milioni 22 669 zilizotumika kununua leseni ya masafa) katika umiliki, mitambo na mali zisizoshikika. Mtaji huu uligharimiwa kwa kutumia fedha zilizozalishwa ndani.

Maelezo zaidi kuhusu umiliki, mitambo na mali zisizoshikika za Kampuni yamewasilishwa katika Maelezo 18 na 19 kwenye taarifa za fedha za pamoja na taarifa binafsi za fedha za kampuni.

Taarifa kuhusu majukumu ya Kampuni zimewasilishwa katika Maelezo 35 katika taarifa za pamoja za fedha na taarifa binafsi za fedha za kampuni.

Mipango ya biashara na maendeleo ya baadaye

Kampuni inalenga kuendeleza uwekezaji katika vichocheo vyake muhimu ambavyo ni data, M-Pesa na huduma kwa wateja wa matumizi ya biashara.

Kampuni tanzu na taasisi zake

Taarifa za fedha za kampuni zinajumuisha taarifa za fedha za kampuni zake tanzu, yaani Vodacom Trust Limited (awali ilijulikana kama M-Pesa Limited) ambayo ni kampuni yenye ukomo kwa udhamini na ina mtaji wa hisa; na Shared Networks Tanzania Limited ('SNT'), Vodacom Tanzania Limited (iliyosajiliwa huko Zanzibar) na M-Pesa Limited, ambazo ni kampuni zenye dhima ya ukomo na mtaji wa hisa. Taarifa za pamoja za fedha pia zinajumuisha taasisi ya M-Pesa yenye muundo wa pamoja, Wadhamini Waliosajiliwa wa M-Pesa ('Trust').

Shughuli kuu ya Vodacom Trust Limited ni kuwa kama wadhamini na/au afisa mwingine yeyote mwenye jukumu la kulinda na kuingia fedha zote zilizopatikana kutokana na/au zinazohusiana na huduma za fedha kwa simu kupitia M-Pesa kwa faida ya watumiaji wa huduma za M-Pesa.

Tarehe 23 Oktoba 2018, jina la kampuni lilibadilishwa kutoka 'M-Pesa Limited' kuwa 'Vodacom Trust Limited' kufuatia kutolewa kwa hati ya kubadili jina iliyotolewa na Wakala wa Usajili na Leseni Tanzania ('BRELA'). Kubadili jina ilikuwa muhimu ili kuwezesha kufuata Sheria ya Mfumo wa Taifa wa Malipo, 2015. Akiba zilizomilikiwa kiudhamini na 'Vodacom Trust Limited' zililhamishiwa kwa wadhamini kulingana na kanuni za Mfumo wa Taifa wa Malipo. Kufuatia hatua hiyo, Vodacom Trust Limited itafungwa.

Tarehe 19 Julai 2016, Kzundi la Kampuni lilinunua 100% ya hisa za SNT. Malipo ya fedha taslimu kiasi cha Shilingi milioni 20 609 (85%) yalilipwa Agosti 2016. Salio lililobaki la Shilingi milioni 3 637 sawa na 15% ya jumla ya gharama yote ya ununuzi lililipwa mwezi Machi 2018. SNT ilikuwa ikitoa huduma za mtandao kwa mauzo ya jumla ambayo ilikuwa na leseni ya kutumia masafa ya 900 MHz katika maeneo ya vijijini hapa Tanzania. Mwaka huu, Vodacom ilipata kibali kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ('TCRA') kutumia masafa ambayo yalikuwa yakimilikiwa na SNT. Wakurugenzi wanakusudia kuifunga SNT baada ya kukamilisha uhamishaji wa mali na madeni yake kwenda Kundi la Kampuni.

Vodacom Tanzania Limited (iliyosajiliwa Zanzibar) ina mtaji wa hisa 100 ambazo hazijalipiwa ambapo hisa 99 zilitolewa kwa Kundi la Kampuni. Kampuni hii imebaki bila kufanya kazi tangu ilipoandikishwa.

2. Rejea maelezo 27 ya Taarifa ya fedha ya Kampuni na kampuni tanzu.
3. Gharama haijajumuisha gharama za leseni ya masafa Shilingi milioni 22 669.

Taarifa ya wakurugenzi inaendelea

M-Pesa Limited iliandikishwa tarehe 26 Oktoba 2018. Kulingana na kanuni za Mifumo ya Taifa ya Malipo ambazo zimeanza kutumika kuanzia Julai 2016, kampuni hii ilituma maombi ya leseni ya kutoa Huduma za Fedha Kielektroniki ('EMI') ambayo ilitolewa na Benki Kuu ya Tanzania ('BoT') tarehe 13 Machi 2019. Kufuatia kupata leseni hiyo, shughuli kuu za kampuni hii itakuwa kutoa huduma za fedha chini ya kanuni za Kutoa Huduma za Fedha Kielektroniki 'EMI' zinazosimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania. Kundi la Kampuni liliendelea kupanga miundo na michakato ya uendeshaji wa kampuni ya M-Pesa. Kampuni hii imeanza kufanya kazi baada ya kipindi tunachotolea taarifa kupita.

Wadhamini wa M-Pesa walisajiliwa chini ya Sheria ya Uandikishaji wa Wadhamini, Sura ya 318 ya Tanzania tarehe 25 Septemba 2019 kwa namba ya usajili 5656. Akiba iliyowekwa kwa uadhamini wa Vodacom Trust Limited iliamishwa kwa Mdamini wa M-Pesa baada ya kipindi tunachotolea taarifa kupita. Mdamini ni taasisi isiyozalisha faida ambayo ina mamlaka ya kutekeleza malengo yake kwa maslahi mapana ya walengwa wa fedha kwenye akaunti za Mdamini. Shughuli za Mdamini zitakuwa pamoja na kusimamia na kuangalia ipasavyo akaunti za mdhamini; kuhakikisha kunakuwa na usalama wa fedha za walengwa kwenye akaunti za mdhamini na kuzilinda dhidi ya hatari kwa kuchukua hatua sahihi za kuweka usalama; kuhakikisha fedha za akaunti ya mdhamini zinatengwa na hazichanganywi na fedha kwa ajili ya shughuli nyingine za EMI.

Kukopa

Hadi kufika tarehe 31 Machi 2020 Kampuni haikuwa na mkopo (2019: Hakuna).

Umiliki wa Kampuni

Vodacom Tanzania Public Limited Company inamilikiwa na kampuni ya Vodacom Group Limited, iliyoandikishwa na yenye makao yake makuu katika Jamhuri ya Afrika Kusini ambayo inamiliki kikamilifu 75.0% (2019: 61.6%) ya hisa za Kampuni zilizotolewa. Pia, kampuni ya Vodacom Group inamilikiwa na kampuni ya Vodafone Group Plc, iliyoandikishwa na makao yake makuu yapo Uingereza.

Miamala ya makampuni washirika

Miamala ya makampuni washirika ilifanyika kwa mtiriko wa kawaida wa kibiashara. Maelezo ya miamala na salio la miamala hiyo yameelezwa katika Maelezo 38 ya taarifa za pamoja za fedha na taarifa za fedha za kampuni binafsi.

Usajili na makao ya kampuni

Kampuni na kampuni zake tanzu zimesajiliwa na makao yake makuu yako katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Wakurugenzi na Katibu wa Kampuni

Wakurugenzi wa Kampuni ambao wamefanya kazi mwaka huu hadi kufikia tarehe ya kutoa taarifa hii ni kama wafuatao:

| Cheo/Jina | Amekuwa kazini tarehe 1 Aprili 2019 | Tarehe ya Uteuzi | Tarehe ya Kustaafu | Anafanya kazi katika tarehe ya kuripoti |
|--------------------------------------|-------------------------------------|------------------|--------------------|---|
| Wakurugenzi | | | | |
| Ali Mufuruki (Mwenyekiti) | ✓ | – | 1 Disemba 2019 | – |
| Andries Delpont* | ✓ | – | – | ✓ |
| Margaret Ikongo (Mwenyekiti wa Muda) | ✓ | 1 Disemba 2019 | – | ✓ |
| Henry Surtees** | ✓ | – | 10 Machi 2020 | – |
| Till Streichert*** | ✓ | – | – | ✓ |
| Thembeke Semane* | ✓ | – | – | ✓ |
| Winifred Ouko^ | ✓ | – | – | ✓ |
| Matimba Mbungela* | ✓ | – | – | ✓ |
| Diego Gutierrez^^ | ✓ | – | – | ✓ |
| Kenneth Gomado^^^ | ✓ | – | – | ✓ |
| Viongozi Watendaji | | | | |
| Hisham Hendi^^^^ | ✓ | – | – | ✓ |
| Jacques Marais* | ✓ | – | – | ✓ |
| Katibu wa Kampuni | | | | |
| Caroline Mduma | ✓ | – | – | ✓ |

* Mwaafrika Kusini ** Mwingereza *** Mjerumani ^ Mkenya ^^ Mbolivia ^^^ Mghana ^^^^^ Mmisri

Wakurugenzi wengine wote ni Raia wa Tanzania.

Maslahi ya wakurugenzi

Wakurugenzi hawana maslahi yoyote ya moja kwa moja katika mtaji wa hisa zilizotolewa za Kampuni au kampuni tanzu yoyote.

Uongozi wa kampuni

Kampuni inahakikisha kuwa huduma za biashara zinatolewa kwa uaminifu, maadili na utaalumu wa hali ya juu. Kanuni za uongozi wa mashirika zinasisitiza kutunza nidhamu, uhuru, haki, uwajibikaji kwa jamii, uwazi na uwajibikaji wa wakurugenzi kwa wadau wote. Kanuni hizi zimeingizwa kwenye taratibu za usimamizi wa ndani na sera zinazoongoza utendaji wa Kampuni.

Bodi ya Wakurugenzi

Bodi inawajibika kwa ujumla katika mafanikio ya Kampuni. Kazi yake ni kuongoza na kufanya maamuzi ya sahihi katika kuelekeza Kampuni kufikia ukuaji endelevu na kuiendesha kwa maslahi ya wanahisa. Wakurugenzi wasio watendaji wanaleta uzoefu na maarifa makubwa waliyo nayo kwenye kamati za Bodi. Kamati zote zinafanya kazi chini ya miongozo iliyopitishwa na Bodi, ambayo huboreshwa mara kwa mara ili kuendana na mabadaliko katika sheria ya mashirika na taratibu bora za uongozi. Bodi imekasimu baadhi ya majukumu yake katika kamati tatu kama inavyoelezwa hapo chini.

Kamati ya Ujira

Kamati ya Ujira inafanya kazi ya kuwezesha na kusaidia Bodi iweze kutekeleza majukumu yake kwa:

- Kupanga na kukubaliana kuhusu ujira na utaratibu wote wa malipo kwa viongozi waandamizi, ukiacha waliotoka kampuni nyingine za Vodacom;
- Kupanga, kukubaliana na kuandaa sera ya ujira ya Kampuni na kuhakikisha inaendana na sera ya ujira ya 'Vodacom Group Limited';
- Kuhakikisha kuwa mikakati na programu zinazozingatia haki na ushindani zinakuwepo ili kuwezesha kuajiri, kutoa motisha na kubakiza wafanyakazi wachapakazi katika ngazi zote ili kusaidia kufanikisha malengo ya kampuni na kulinda maslahi ya wanahisa;
- Kupitia na kupendekeza kwenye Bodi vigezo muhimu vya kupima ufanisi wa viongozi waandamizi katika kutekeleza kazi na majukumu yao; na
- Kuandaa na kutekeleza falsafa ya sera ya ujira.

Kamati ya Uteuzi

Kamati ya Uteuzi inafanya kazi ya kuwezesha na kusaidia Bodi kutekeleza majukumu yake kwa:

- Kuzingatia maslahi au mipango yenye maslahi thabiti ya kifedha;
- Kuhakikisha kuwa ufanisi wa wajumbe wa Bodi unatathminiwa;
- Kupitia sera za kupandisha vyeo, kuhamisha na kusitisha ajira kwa ajili ya Kampuni;
- Kufuatilia ukubwa na muundo wa wajumbe wa Bodi;
- Kutathmini kila mwaka uhuru wa wakurugenzi katika kutekeleza majukumu yao;
- Kupendekeza watu wa kuteuliwa kama wajumbe wa Bodi na kamati zake;
- Kupitia mipango ya Bodi ya kupokezana madaraka;
- Kutathmini muundo na ufanisi wa bodi za kampuni tanzu;
- Kupitisha uteuzi wa watu kwenye bodi za kampuni tanzu;
- Kuhakikisha kama wajumbe wa Bodi wana sifa stahili kwa nafasi zao;
- Kupitia muundo wa Kampuni ili kuhakikisha kuwa unafaa kutekeleza mkakati na malengo ya muda mrefu ya kibiashara; na
- Kuhakikisha sheria na kanuni husika zinafuatwa.

Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji (ARCC)

Kamati hii ina wajibu wa:

- Kupitia matokeo ya muda ya pamoja, matokeo ya awali, taarifa za mwaka na taarifa za pamoja za fedha za Kampuni na taarifa za fedha za kampuni kibinafsi;
- Kufuatilia utekelezaji wa sheria husika na Kanuni za Soko la Hisa la Dar es Salaam;
- Kuripoti kwenye Bodi kuhusu usahihi na ubora wa sera na taratibu za hesabu za Kampuni, ikijumuisha sera na taratibu muhimu za uhasibu;
- Kusimamia michakato ya kutoa taarifa za mwaka za fedha;
- Kutathmini uteuzi na/au kusitisha huduma ya wakaguzi wa nje, pamoja na ada zao za ukaguzi, uhuru na uhalali mchakato wa ukaguzi na kuamua aina huduma nyingine zisizo za kikaguzi;
- Kupitisha mpango wa ukaguzi wa ndani wa mwaka;
- Kupokea na kushughulikia ipasavyo malalamiko, ya nje na ndani, yanayohusiana na taratibu za uhasibu na ukaguzi wa ndani au kuhusu maudhui au ukaguzi wa kampuni zote zilizo ndani ya taarifa za pamoja za fedha za Kampuni au masuala husika;
- Kupitia na kufuatilia namna ya kushughulikia na kuripoti masuala yanayohusiana na kodi;
- Kufuatilia shughuli na michakato ya usimamizi wa dharura na kutathmini dharura muhimu zaidi za Kampuni; na
- Kufuatilia ufanisi wa michakato ya kuamsha ufahamu na kujenga uelewa wa sheria na kanuni husika ili kuhakikisha kuwa menejimenti inazitekeleza.

Taarifa ya wakurugenzi inaendelea

Michango ya Kisiasa na Kujitolea

Kampuni haikutoa michango yoyote ya kisiasa mwaka huu (2019: hakuna).

Kampuni ilitoa michango kwa Vodacom Tanzania Foundation jumla Shilingi milioni 315 katika mwaka huu (2019: Shilingi milioni 600).

Wajibu wa kampuni kwa jamii

Vodacom Tanzania Foundation ('Foundation') ni kampuni yenye dhima ya ukomo kwa dhamana iliyosajiliwa na yenye makao yake katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Sheria ya Makampuni, 2002 Sura ya 212 ya sheria za Tanzania.

Kufuatia marekebisho ya Sheria ya Makampuni, 2002 na Sheria iliyofanyiwa Marekebisho Madogo, No. 3 ya 2019 ambayo imeanza kutumika tarehe 30 Juni 2019, mamlaka ya kusajili makampuni ambayo yanakataza kugawana faida na ambayo hayakusudii kuendesha biashara, yalihamishwa kutoka BRELA kwenda kwa Msajili wa Asasi Zisizo za Kiserikali ('AZISE'). Vilevile, BRELA ilitoa tangazo kwa umma linaloeleza kuwa kuanzia tarehe 30 Agosti 2019, Msajili wa Makampuni hatatunza kwenye masjala yake kumbukumbu za kampuni yoyote ambayo hairuhusiwi kugawa faida na haikusudii kufanya biashara, na wakashauri kampuni zilizoguswa na mabadiliko hayo kuwasiliana na Msajili wa AZISE ili wapatiwe mwongozo na maelekezo kuhusiana na usajili wa AZISE kulingana na Sheria ya Marekebisho Madogo, Na. 3 ya 2019.

Kampuni ya Vodacom Foundation iliathiriwa na mabadiliko haya katika sheria kwa kuwa iliandikishwa kama kampuni yenye dhima ya ukomo kwa udhamini isiyokuwa na malengo ya kutengeneza faida. Hivyo ilifutwa kwenye Usajili wa Makampuni tarehe 30 Agosti 2019. Taasisi mbadala itwayo Vodacom Tanzania Foundation, ilisajiliwa na Msajili wa AZISE katika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mujibu wa Sheria ya Asasi Zisizokuwa za Kiserikali ya 2002 (iliyorekebisha mwaka 2005) na Kanuni za Asasi Zisizokuwa za Kiserikali (Imerekebisha) ya 2018 (pamoja, Sheria na Kanuni za AZISE) za Tanzania.

Vodacom Foundation ni 'mkono' wa uwajibikaji kwa umma wa Kampuni. Madhumuni yake ni kuleta manufaa kwa umma kupitia matumizi ya teknolojia ya simu za kiganjani ili kuboresha maisha ya jamii. Vodacom Foundation inashirikiana na AZISE za ndani, asasi za kiraia, asasi za kijamii na mashirika yasiyozalisha faida kuunga mkono juhudi za serikali katika kuboresha elimu, afya na ushirikishwaji kifedha kwa kulenga vikundi vya watu walio katika mazingira magumu.

Vodacom Foundation imewekeza Shilingi milioni 16 150 (2019: Shilingi milioni 15 800) tangu ilipoanza kutoa mchango wa kuboresha jamii ya Tanzania.

Tahadhari ya Madeni

Masuala ya kodi

Tozo ya kodi siku zijazo, kiwango cha kodi na faida kabla ya kodi ni mambo yanayoweza kuathiriwa na sababu mbalimbali ambazo ni pamoja na marekebisho ya mfumo wa kodi yanayofanyika nchini na utatuzi wa migogoro ya kodi iliyopo na Mamlaka ya Kodi Tanzania ('TRA' au 'mamlaka ya kodi') na/au mahakama za kodi.

Kampuni imekuwa na inadhamiria kuendelea kushughulikia masuala yote ya kodi kwa uaminifu na uwazi katika ikiwa ni pamoja na sera ya uwazi katika mamlaka ya kodi na ulipaji wa kodi zote zinazotakiwa kulipwa kwa mujibu wa sheria husika za kodi nchini Tanzania.

Kampuni hufanyiwa ukaguzi mara kwa mara na kukadiriwa na mamlaka ya mapato kuhusu taarifa zake za kodi ya mapato na kodi nyinginezo. Matokeo ya mapitio hayo ni kuwa katika baadhi ya matukio, migogoro inaweza kutokea na mamlaka ya mapato kuhusu tafsiri au matumizi ya kanuni fulani za kodi ambapo sheria hizi za kodi zina maana nyingi na zinaweza kuwa na mawanda mapana ya tafsiri.

Ili kushughulikia na kudhibiti hali ya uwezekano wa mambo ya kodi kuwa na tafsiri zinazotofautiana na hivyo kukosa uhakika wa usahihi, utawala bora ni muhimu kutumika ili kuwa na biashara endelevu. Hivyo, misimamo mikuu ya kodi iliyochukuliwa hupitiwa na uongozi na kutolewa taarifa kwenye Bodi. Kampuni hutumia msaada wa washauri wa nje wa kodi ambao huunga mkono msimamo uliochukuliwa kuhusiana na masuala muhimu ya kodi kuhusu matumizi na tafsiri ya sheria ya kodi.

Kampuni imezingatia masuala yote ya migogoro na mamlaka ya kodi na kuripoti katika vitabu na taarifa za fedha uwezekano wowote wa madeni ya ziada kutokana na masuala ya kodi palipo na uwezekano wa hilo kutokea, wakati migogoro bado ikisuluhishwa. Kampuni haitoi taarifa zote kwa undani zinazohusu migogoro ya kodi iliyopo kwa sababu masuala hayo bado yapo katika mchakato wa usuluhishi.

Ifuatayo ni migogoro iliyopo ya kodi ambayo inaweza ikasababisha madeni ya kikodi ikiwa Kampuni itashindwa katika mashauri yake. Athari za kifedha za migogoro hiyo hazijajumuishwa kama sehemu ya taarifa hii ya fedha.

- **Punguzo la kodi kutokana na uchakavu wa mitambo**

Migogoro iliyopo ya kodi inayohusu uainishaji wa vifaa vya mawasiliano ya simu kwa ajili ya ukokotoaji wa kodi bado ipo mahakamani. TRA haikubaliani na namna Kampuni ilivyotafsiri uainishaji wa vifaa vya mawasiliano ya simu kulingana na Sheria ya Kodi ya Mapato. Hata hivyo, suala hili linahusu tofauti ya wakati wa kutambua punguzo la kodi.

• Kodi ya zuio katika huduma za setilaiti, kuzuru kimataifa na mkongo uliopita chini ya bahari

Makadirio yaliyopokelewa na kampuni kuhusiana na kodi ya zuio katika huduma za setilaiti, kuzuru kimataifa na huduma za mkongo uliopita chini ya bahari zilizotolewa na watoa huduma wa kimataifa, pia yapo katika mchakato mahakamani.

Kampuni haikukata kodi ya zuio kwenye malipo yaliyofanywa kwa watoa huduma wa kimataifa wa huduma hizi za mawasiliano ya simu kwa kuwa Tanzania ni mwanachama wa 'International Telecommunication Union' (ITU) na imesaini makubaliano na ITU ambayo yanaondoa tatizo la kutozwa kodi mara mbili kwa huduma za mawasiliano ya simu. Kampuni imetoa ushahidi (uthibitisho) wa makubaliano hayo baina ya ITU na Tanzania.

• Usahihi wa Bei za huduma kutoka kwa kampuni washirika

Kampuni, ikiwa ni sehemu ya kampuni ya kimataifa, inatumia sana huduma zinazotolewa na kampuni washirika kwa namna ambayo inaongeza ufanisi, huku miamala ya huduma hizi ikifanyika kwa kanuni za soko. Miamala hii imeandikwa katika nyaraka za Kampuni zinazohusu bei za huduma kutoka kwa kampuni washirika kwa mujibu wa kanuni za ndani na miongozo ya OECD. TRA imefanya ukaguzi wa miamala hiyo kwa kipindi kati mwaka 2015 hadi 2017 ambapo baadhi ya vipengele vimekuwa na mgogoro kuhusu njia iliyotumika na namna vipengele vingine vya kanuni za kukubalina bei ya huduma kwa kampuni washirika, vilivyotumika.

Mashauri yaliyo mahakamani na madai mengine

Kwa sasa Kampuni ina mashauri mbalimbali ya kisheria yaliyo mahakamani na imetathmini matokeo ya mashauri hayo kwa kushauriana na mshauri wake wa kisheria. Kufuatia tathmini hii, menejimenti ya Kampuni imeridhika na hatua zilizochukuliwa ikiwemo tahadhari ya madeni kwenye vitabu vya fedha kuhusiana na mashauri haya.

Kampuni pia ina mashtaka ya madai kutokana na mikataba mbalimbali iliyoingia na wabia wake wa biashara. Migogoro inaweza ikaibuka kuhusiana na tafsiri au matumizi ya vifungu vya makubaliano ya mkataba. Migogoro hii inaweza ikaamuliwa kinyume na matarajio ya Kampuni na hivyo kuisababisha Kampuni kuwajibika. Menejimenti imetathmini kuwa hakuna uhakika wa kutosha katika madai yaliyopo, unaolazimu Kampuni kurekodi tahadhari ya madeni ambayo inaweza kulazimika kuyalipa. (2019: Hakuna).

Masuala mengine

Usajili wa wateja kwa alama za vidole

Mnamo tarehe 1 Mei 2019, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ilitoa miongozo mipya inayoagiza kuwa usajili halali wa wateja ni ule wa kutumia Namba ya Kitambulisho cha Taifa (NIN) kilichotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA). TCRA iliagiza usajili kwa kutumia eKYC usitishwe. Kampuni kwa kushirikiana na wadau wengine katika sekta imeendelea kushirikiana na TCRA kuhakikisha inatekeleza maelekezo ya kanuni hizo mpya za usajili. Makampuni ya simu kwa kushirikiana na TCRA na NIDA yalizindua kampeni nchini kote kuielimisha jamii ili kuharakisha usajili kwa utaratibu huu mpya.

Mchakato wa usajili kwa alama za vidole ulianza mwezi Mei 2019, na kutakiwa kukamilika ifikapo Desemba 2019, na baadaye muda uliongezwa hadi tarehe 20 Januari 2020. Idadi ndogo ya watu waliokuwa na Vitambulisho vya Taifa nchini kote uliathiri mchakato huo. Hadi kufikia tarehe 20 Januari 2020, Kampuni haikuwa imekamilisha usajili kwa baadhi wateja ambapo TCRA iliagiza kusitishwa kwa awamu, huduma za simu kwa wateja ambao hawajakamilisha usajili. Hii ilipelekea Vodacom kuwafungia huduma wateja milioni 2.9 kati ya tarehe 20 Januari na tarehe 31 Machi 2020. Mpaka kufikia mwisho wa mwaka wa fedha, wateja wengine milioni 2.5 walikuwa bado hawajasajiliwa na hivyo wanatarajiwa kufungwa huduma za simu kwa mujibu wa maagizo ya TCRA, hadi hapo usajili wao utakapokamilika.

Zoezi hili liliathiri mapato ya Kampuni katika robo ya nne ya mwaka wa fedha, na mapato ya mwaka kwa ujumla. Na hili pamoja na ongezeko la gharama zilizotumika katika mchakato wa kusajili upya laini za simu, vimeathiri matokeo ya kifedha ya Kampuni. Kampuni inaendelea na mchakato wa kusajili laini za simu ambazo hazijasajiliwa kwa kushirikiana na TCRA na wenzetu katika sekta kuhakikisha laini zote za simu zinasajiliwa upya. Ingawa hatua zote muhimu zinachukuliwa, athari za wateja ambao hawajasajiliwa na wamesitishiwa huduma, zina athiri ufanisi wa kifedha wa Kampuni.

Mabadiliko mengine katika kanuni za usajili wa laini za simu

Tarehe 7 Februari 2020, Serikali ilichapisha Kanuni mpya za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Usajili wa Laini za Simu) 2020. Kanuni hizo zimeeleza mchakato wa usajili kwa alama za vidole kwa kutumia kitambulisho cha Taifa, kama utambulisho pekee kwa usajili wa laini za simu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kanuni hizi pia zimeweka ukomo wa idadi ya laini za simu zinazoweza kumilikiwa na mtu binafsi na kampuni au taasisi kuanzia tarehe 1 Julai 2020. Mtu binafsi haruhusiwi kumiliki zaidi ya laini moja ya simu kwa ajili ya matumizi ya huduma za sauti, ujumbe wa maneno na data na si zaidi ya laini nne za simu kwa matumizi ya mawasiliano ya mashine kwa mashine kutoka kwa kila mtoa huduma ya mawasiliano ya simu. Kampuni au taasisi hairuhusiwi kuwa na zaidi ya laini thelathini za simu kwa ajili ya huduma ya sauti, ujumbe wa maneno na data na si zaidi ya laini hamsini za simu kwa mawasiliano ya mashine kwa mashine kutoka kwa kila mtoa huduma ya mawasiliano ya simu. Inatakiwa kupata kibali cha TCRA ili kumiliki laini za simu za ziada. Kampuni na watoa huduma wengine wa mawasiliano ya simu wanashirikiana na TCRA kuweka mfumo wa kiotomatiki ambao utawawezesha wateja kupata kibali cha kumiliki laini za simu za ziada kwa urahisi.

Taarifa ya wakurugenzi inaendelea

Viwango vya tozo kwa simu zinazolingia/kutoka kwenye mitandao mingine ya ndani

TCRA ilichapisha viwango vipya vya kuunganisha mitandao mingine (MTRs) tarehe 29 Desemba 2017 ambavyo vimeanza kutumika kuanzia Januari 2018 hadi Desemba 2022. Matokeo yake, viwango vya MTR vimepungua kuanzia Shilingi 10.4 hadi Shilingi 5.2 kuanzia Januari 2020 (kutoka Shilingi 15.6 hadi Shilingi 10.4 kuanzia Januari 2019). Njia nyiririko ya TCRA inapunguza MTR kila mwaka hadi itakapofika Shilingi 2.00 mwezi Januari 2022. Rufaa ya Kampuni dhidi ya MTR mpya iliyofunguliwa kwenye Mahakama ya Ushindani Tanzania (FCT) ilisikilizwa mnamo Desemba 2019 na uamuzi haukuwa upande wetu.

Ununuzi wa hisa za Mirambo Limited

Mwanahisa mkubwa, Vodacom Group Limited, amenunua hisa milioni 588 za Kampuni zilizokuwa zikimilikiwa hapo awali na Mirambo Limited ('Mirambo'). Ununuzi huu umesababisha Vodacom Group Limited kuongeza jumla ya umiliki wake kwenye Kampuni kutoka 61.6% (moja kwa moja na kwa njia nyingine) hadi 75% (moja kwa moja). Muamala ulifanyika mwaka huu baada ya kukamilisha masharti yaliyokuwepo, ikiwa ni pamoja na kupata vibali husika.

Matukio baada ya muda wa ripoti hii

Matukio baada ya muda wa ripoti hii yameelezwa katika Maelezo 45 katika taarifa za pamoja za fedha na taarifa binafsi za fedha za kampuni. Bodi haina taarifa ya suala au mazingira mengine yoyote yaliyoibuka tangu mwisho wa muda wa kuripoti ambayo yalipaswa kushughulikiwa katika taarifa hii, na kuhitaji kufanyiwa marekebisho au kufafanuliwa kwenye taarifa za pamoja au binafsi za fedha.

Mkaguzi wa hesabu

Ernst & Young, mkaguzi wa hesabu kwa mwaka wa fedha 2020, ameonyesha utayari wa kuendelea kufanya kazi nasi na anastahili kuteuliwa tena. Azimio la kupendekeza kuteuliwa tena kwa Ernst & Young kama mkaguzi wa hesabu za Kampuni kwa mwaka unaoishia tarehe 31 Machi 2021 litapelekwa kwenye Mkutano Mkuu wa Mwaka.

Taarifa za pamoja za fedha na taarifa binafsi za fedha za kampuni

Taarifa za fedha za kampuni na kampuni tanzu kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2020 zilipitishwa na kuidhinishwa na Bodi kutolewa tarehe 21 Mei 2020.

Kwa agizo la Bodi



Margaret Ikongo
Mwenyekiti wa Muda



Hisham Hendi
Mkurugenzi

Tamko la majukumu ya wakurugenzi

Kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2020

Sheria ya Makampuni, 2002 Na.12 ya Tanzania inawataka wakurugenzi kuandaa taarifa za pamoja za fedha na taarifa za fedha za kampuni moja moja kwa kila mwaka wa fedha ambazo zinaonyesha ipasavyo hali ya kifedha na matokeo ya Kampuni tanzu na Kampuni. Wakurugenzi pia wanatakiwa kuhakikisha kuwa Kampuni na Kampuni Tanzu zinatunza kumbukumbu sahihi za hesabu za fedha ambazo zinaeleza kwa usahihi wa kutosha, hali ya kifedha na matokeo kwa Kampuni na Kampuni Tanzu. Wakurugenzi pia wana jukumu la kulinda mali za Kampuni na Kampuni Tanzu na kuchukua hatua madhubuti za kuzuia na kugundua ulaghai, makossa yasiyo kusudiwa na mambo mengine yasiyo sawa.

Wakurugenzi wanakubali wajibu wa kuandaa taarifa za fedha za Kampuni na Kampuni tanzu, ambazo zimeandaliwa kwa kuzingatia sera sahihi za uhasibu zikichangiwa na maamuzi na makadirio ya kimantiki, kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Kuripoti Masuala ya Kifedha (IFRS) na masharti ya Sheria ya Makampuni Na 12, ya mwaka 2002. Wakurugenzi wanaamini kuwa taarifa za fedha za Kampuni na Kampuni tanzu zinawasilisha kwa usahihi, katika hali zote, hali ya kifedha na matokeo ya kifedha ya kampuni hizo kulingana na kanuni za IFRS na masharti ya Sheria ya Makampuni, Na 12, ya mwaka 2002. Wakurugenzi pia wanakubali wajibu wa kutunza kumbukumbu za fedha ambazo zinaweza kutegemewa katika maandalizi ya taarifa za fedha za Kampuni na Kampuni tanzu na vilevile kuandaa, kutekeleza na kusimamia uwepo wa mazingira ya usimamizi wa ndani unaoweza kuandaa na kuwasilisha taarifa za fedha ambazo hazina upotoshaji utokanao na udanganyifu au makosa yasiyokusudiwa.

Hakuna dalili yoyote ambayo wakurugenzi wameiona inayoashiria kuwa Kampuni na Kampuni tanzu hazitaweza kuendelea na shughuli zake za biashara ndani ya kipindi cha walau miezi kumi na miwili ijayo kutoka tarehe ya tamko hili.

Taarifa ya fedha ya Kampuni na Kampuni tanzu kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2020 zilithibitishwa na kuidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi tarehe 21 Mei 2020.



Margaret Ikongo
Mwenyekiti wa Muda



Hisham Hendi
Mkururugenzi

Tamko la mkuu wa kitengo cha fedha

Kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2020

Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA) kulingana na mamlaka yaliyotolewa kwake na Sheria ya Wakaguzi na Wahasibu (Usajili) Na. 33 ya 1972, kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 2 ya 1995, inataka tamko la Mkuu wa Kitengo cha Fedha ambaye anayehusika na maandalizi ya taarifa za fedha ya kampuni husika yaambatanishwe na taarifa za fedha.

Ni wajibu wa mtaalamu wa uhasibu kuisaidia Bodi ya Wakurugenzi kutekeleza wajibu wa kuandaa taarifa za fedha za kampuni zikionesha muonekano sahihi wa hali ya kifedha na ufanisi kwa mujibu wa IFRS na masharti ya Sheria ya Makampuni, 2002 Na.12.

Jukumu kamili la kisheria la kuandaa taarifa za fedha lipo kwa Bodi ya Wakurugenzi kama ilivyoielezwa katika Tamko la Majukumu ya Wakurugenzi katika ukurasa uliotangulia.

Mimi, Robin Kimambo, nikiwa Mkuu wa Kitengo cha Fedha wa Vodacom Tanzania Public Limited Company ninakiri jukumu langu la kuhakikisha kuwa taarifa za fedha za kampuni na kampuni tanzu kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2020 zimeandaliwa kwa mujibu wa IFRS na masharti ya Sheria ya Makampuni, 2002 Na.12 ya Tanzania.

Hivyo ninathibitisha kuwa taarifa za fedha za kampuni na kampuni tanzu zinaonesha kwa usahihi hali ya kifedha ya Vodacom Tanzania Public Limited Company kwa tarehe hiyo na kuwa wameiandaa kwa kutumia kumbukumbu za fedha zilizotunzwa kwa usahihi.



Robin Kimambo
Namba ya Uanachama wa NBAA: GA4810
Mkuu wa Masuala ya Fedha

21 Mei 2020

Taarifa ya Mkutano Mkuu

Vodacom Tanzania Public Limited Company

(Imesajiliwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)

(Namba ya usajili 38501)

(ISIN: TZ1996102715 Ticker code: VODA)

('Vodacom Tanzania' au 'Kampuni')

Taarifa inatolewa kuwa mkutano mkuu wa nne wa Kampuni kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2020 utafanyika siku ya Jumatano tarehe 30 Oktoba 2020, kwa njia ya kielektroniki kuanzia saa nne asubuhi. Mkutano huu utajadili yafuatayo:

1. Kuthibitisha kumbukumbu

Kuthibitisha kumbukumbu za mkutano mkuu wa tatu uliofanyika tarehe 20 Septemba 2019.

Azimio la kawaida namba 1

"ILIAMULIWA KUWA kumbukumbu za mkutano mkuu wa tatu uliofanyika tarehe 20 Septemba 2019 zimethibitishwa."

Nakala za kumbukumbu zinapatikana kwenye tovuti ya Kampuni www.vodacom.co.tz/investors

2. Kupitisha taarifa za fedha za mwaka zilizokaguliwa

Kupokea, kujadili na kupitisha taarifa za fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2020.

Azimio la kawaida namba 2

"ILIAMULIWA KUWA taarifa ya fedha zilizokaguliwa za Kampuni ikijumuisha kampuni zake tanzu, pamoja na ripoti ya wakaguzi huru na ya wakurugenzi kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2020, zimepokelewa na kupitishwa."

Taarifa ya mwaka inapatikana katika tovuti ya Kampuni www.vodacom.co.tz/investors

3. Uchaguzi wa wakurugenzi

Kwa kupitia maazimio tofauti:

- 3.1 Ndg. Nkateko Nyoka, Ndg. Sitholizwe Mdlalose na Ndg. Dejan Kastelic waliteuliwa kwa mujibu wa kifungu cha 86 cha Katiba ya Kampuni kujaza nafasi zilizojitokeza katika Bodi na kuendelea kutekeleza majukumu ya kiofisi hadi mkutano wa kawaida unaofuata, na hivyo wanastahili kuchaguliwa tena.

Azimio la kawaida namba 3

"ILIAMULIWA KUWA Ndg. Nkateko Nyoka amechaguliwa kuwa mkurugenzi asiye mtendaji."

Azimio la kawaida namba 4

"ILIAMULIWA KUWA Ndg. Sitholizwe Mdlalose amechaguliwa kuwa mkurugenzi asiye mtendaji."

Azimio la kawaida namba 5

"ILIAMULIWA KUWA Ndg. Dejan Kastelic amechaguliwa kuwa mkurugenzi asiye mtendaji."

Ufuatao ni wasifu wa Ndg. N Nyoka, Ndg. S Mdlalose na Ndg. D Kastelic:

Nkateko Nyoka (57)

Afisa Mkuu wa Sheria, Kanuni na Dharura – Vodacom Group Limited

Shahada ya Uzamili ya Sheria na Utawala wa Umma kutoka Chuo Kikuu cha Harvard

Shahada ya Sheria pamoja na cheti cha uwakili (Baccalaureus Procurationis (B.Proc)) kutoka Chuo cha Witwatersrand, Johannesburg

Bw Nyoka ni Afisa Mkuu wa Sheria, Kanuni na Dharura wa Vodacom Group Limited, Afrika Kusini. Kabla ya kujiunga na Vodacom Group, alishika nyadhifa mbalimbali za uongozi MTN (Pty) Limited na MTN Group Limited pamoja Taasisi ya Jamii ya MTN, Afrika Kusini. Pia Bw Nyoka alikuwa Afisa Mkuu Mtendaji wa kampuni ya Independent Communications Authority of South Africa (ICASA) ambapo alitoa mchango mkubwa uliowezesha mazingira ya ushindani katika sekta ya mawasiliano ya Afrika ya Kusini. Bw Nyoka pia ni mkurugenzi wa bodi ya Vodacom Lesotho, Vodacom Msumbiji na Vodacom DRC.

Sitholizwe Mdlalose (40)

Kaimu Afisa Mkuu Fedha wa – Vodacom Group Limited

*Shahada ya Uhasibu (BCompt) kutoka Chuo Kikuu cha Afrika ya Kusini
Cheti cha taaluma ya uhasibu (ACCA)*

Bw. Mdlalose ni Mkurugenzi wa fedha wa Vodacom South Africa (VSA), Afrika Kusini tangu 2017. Bwana Mdlalose amewahi kuwa Afisa mkuu wa fedha wa biashara za kimataifa na Afisa mtendaji mkuu ukaguzi wa mahesabu ya ndani wa Vodacom Group. Kabla ya kujiunga na Vodacom Group Bw Mdlalose alifanya kazi kwa zaidi ya miaka 6 na Vodafone Group akishikilia nyadhifa mbalimbali. Ana zaidi ya miaka 19 katika fani ya usimamizi na ushauri wa fedha; ambayo miaka 13 akiwa katika sekta ya mawasiliano ya simu.

Dejan Kastelic (43)

Afisa Mkuu wa Teknolojia – Vodacom Group Limited

*Shahada ya Sayansi katika Uhandisi Umeme kutoka Chuo kikuu cha Maribo kilichopo Slovenia
Alisoma Chuo Kikuu cha Harvard kilichoko Boston Marekani na INSEAD.
Amejiunga katika program ya Usimamizi wa Biashara huko IEDC Bled*

Bw. Kastelic aliteuliwa kuwa Afisa Mkuu wa Teknolojia wa Vodacom Group, Afrika Kusini mwezi Agosti 2020. Kabla ya kujiunga na Vodacom, alikuwa Afisa Mkuu wa Teknolojia na Habari katika kampuni ya PT Indosat Ooredoo TBK, sehemu ya kampuni ya Kundi la makampuni ya Ooredoo huko Qatar. Aidha, aliwahi kuwa Mkurugenzi wa kampuni ya Indosat, Singapore na ni Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya Usimamizi wa Posta Slovenije d.o.o. Bw Kastelic alianza kazi katika kampuni ya simu Amis Ltd hadi kufikia nafasi ya Afisa Mkuu wa Teknolojia. Mwaka 2009 alihamia kampuni ya IBM Ulaya Mashariki na Kati kama Meneja Usimamizi wa Rasilimali. Mwaka 2012 alijiunga na kampuni ya Telekom Austria akiwa kama Mkurugenzi Mtendaji na Afisa Mkuu wa Teknolojia na Habari na baadaye akawa Mkurugenzi wa Kundi na Afisa Mkuu wa Teknolojia na Habari akisimamia kampuni za simu – Vip mobile, Serbia na Si.Mobil Slovenia. Mwaka 2015, alihamishiwa kampuni ya Mobitel Bulgaria hadi alipoteuliwa kwenye nafasi aliyoshikilia mwanzo katika kampuni ya Indosat. Bw Kastelic pia ni mkurugenzi wa bodi ya Vodacom Msumbiji na Vodacom Lesotho.

- 3.2 Ndg. Winifred Ouko and Ndg. Thembeke Semane wanastahili kustaafu katika mkutano huu mkuu kwa mujibu wa vifungu 104 na 105 vya Katiba ya Kampuni. Vifungu hivyo vinabainisha kuwa licha ya kustaafu, wanaweza kuchaguliwa kwa mara nyingine tena kuwa wakurugenzi.

Azimio la kawaida namba 6

“LIAMULIWA KUWA Ndg. Winifred Ouko amechaguliwa tena kuwa mkurugenzi huru wa Kampuni.”

Azimio la kawaida namba 7

“LIAMULIWA KUWA Ndg. Thembeke Semane amechaguliwa tena kuwa mkurugenzi huru wa Kampuni.”

Ufuatao ni wasifu wa Ndg. W Ouko, Ndg. T Semane:

Winifred Ouko (50)

Mkurugenzi huru

Mwenyekiti Kamati ya Ujira

Mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji na anachukuliwa kuwa mtaalamu wa fedha katika kamati hii

*Shahada ya Uzamili katika Usimamizi wa Biashara, Chuo Kikuu cha Cornell, United States of America.
Mwanachama wa Taasisi ya Taaluma ya Uhasibu, Kenya.*

Winnie aliteuliwa kuwa mkurugenzi huru wa Vodacom Tanzania mwezi Novemba 2017. Winnie ana uzoefu mkubwa katika masuala fedha katika makampuni na miradi. Winnie ni Mkurugenzi Mtendaji wa Lattice Consulting, akiwa na uzoefu wa zaidi ya miaka 20 wa kutoa huduma za ushauri katika masuala ya fedha, pamoja na mikakati na mafunzo kwa wateja ndani ya Afrika na Amerika Kaskazini. Winnie ni mkurugenzi asiye mtendaji na mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi na Dharura ya Benki ya Absa, Kenya. Pia ni mjumbe wa bodi ya Kenya Pooled Water Fund.

Thembeke Semane (44)

Mkurugenzi huru

Mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji na anachukuliwa kuwa mtaalamu wa fedha kwa madhumuni ya kamati hii

Stashahada ya Juu katika Usimamizi wa Biashara, Chuo Kikuu cha Biashara cha Pretoria Gordon, Afrika Kusini Mwanachama wa Taasisi ya Taaluma ya Benki ya Afrika Kusini.

Thembeke aliteuliwa kuwa mkurugenzi huru wa Vodacom Tanzania mwezi Novemba 2017. Thembeke ana uzoefu katika masuala ya biashara ukihusisha mikakati ya mashirika, utekelezaji wa mifumo ya biashara, miradi yenye thamani kubwa, utekelezaji na ufuatiliaji, utawala bora na vilevile usimamizi wa fedha. Thembeke ni mkurugenzi wa Linea Consulting (Pty) Ltd, mjumbe wa Kamati ya Udhhibiti ya ACASA & ATNS, akiripoti kwa Waziri wa Usafirishaji wa Afrika Kusini na pia ni mjumbe wa Baraza la ICASA. Thembeke anafanya kazi kama mjumbe wa bodi wa Idara ya Makazi EAAB, Mwenyekiti wa Kamati yake ya Fedha na Uwekezaji na ni mjumbe wa Kamati za Ukaguzi na Dharura pamoja na ya Rasilimali Watu na Ujira. Pia ni mjumbe wa bodi na mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi na Usimamizi wa Dharura na Kamati ya Ujira ya Mbuga za Wanyama za Afrika Kusini. Vilevile, Thembeke ni mjumbe wa South African Heritage Resource Agency na Kamati ya Udhhibiti na Usimamizi wa Utendaji wa Manispaa ya Sol Platje.

4. Uteuzi wa Ernst & Young kuwa wakaguzi huru wa Kampuni

Kuteua kampuni ya Ernst & Young Inc., kama ilivyopendekezwa na Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji, kuwa wakaguzi huru wa Kampuni na kushikilia nafasi hiyo hadi mwisho wa mkutano mkuu ujao wa mwaka.

Azimio la kawaida namba 8

"ILIAMULIWA KUWA Ernst & Young Inc. wameteuliwa kuwa wakaguzi huru wa Kampuni na kushikilia nafasi hiyo hadi mwisho wa mkutano mkuu ujao wa mwaka."

5. Uteuzi wa wajumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji

Kupitia maazimio tofauti na kwa mujibu wa kifungu cha 32(f) cha Katiba ya Kampuni, Ndg. Margaret Ikongo, Ndg. Thembeke Semane na Ndg. Winifred Ouko wakiwa wajumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji wachaguliwe kuendelea kuwa wajumbe wa kamati tajwa.

Azimio la kawaida namba 9

"ILIAMULIWA KUWA Ndg. Winifred Ouko amechaguliwa kuendelea kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji."

Azimio la kawaida namba 10

"ILIAMULIWA KUWA Ndg. Thembeke Semane amechaguliwa kuendelea kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji."

Azimio la kawaida namba 11

"ILIAMULIWA KUWA Ndg. Margaret Ikongo amechaguliwa kuendelea kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji."

Wasifu wa Ndg. Margaret Ikongo, Ndg. Winifred Ouko na Ndg. Thembeke Semane umeonyeshwa ukurasa wa 37 na 38.

Margaret Ikongo (62)

Mkurugenzi huru

Mwenyekiti Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji na anatambuliwa kuwa mtaalamu wa fedha kwa madhumuni ya kamati hii

Shahada ya Uzamili katika Usimamizi wa Biashara na masuala ya Fedha, Chuo Kikuu Huria Tanzania.

Cheti cha Kimataifa cha Usimamizi wa Viashiria Hatarishi, Taasisi ya Usimamizi wa ViashiriaHatarishi, Uingereza.

Diploma ya Kimataifa ya Usimamizi wa Viashiria Hatarishi na Mjumbe Mhitimu wa Taasisi ya Usimamizi wa ViashiriaHatarishi, Uingereza. Mjumbe katika Taasisi ya masuala ya Bima, Uingereza.

Margaret aliteuliwa kuwa mkurugenzi huru wa Vodacom Tanzania mwezi Novemba 2017. Pia ni mjumbe wa bodi ya wakurugenzi ya NMB Bank PLC na AAR Insurance Tanzania. Kabla ya hapo, Margaret alikaa kwenye Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF). Margaret ana uzoefu mkubwa katika masuala ya fedha na utawala bora akiwa ameupata kutokana na kufanya kazi katika tasnia ya bima ambapo alikuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Bima la Taifa kwa kupindi cha miaka kumi. Margaret pia alikuwa mshauri wa Kamishna wa Mamlaka ya Udhhibiti wa Bima Tanzania pamoja na Kaimu Mkuu wa Kurugenzi ya Ufundi.

6. Gawio

6.1 Gawio la mwisho

Kuidhinisha gawio la mwisho la Shi 12.26 kwa kila hisa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Machi 2020 kama ilivyopendekezwa na wakurugenzi. Gawio litalipwa kabla au Ijumaa ya tarehe 13 Novemba 2020 kwa wanahisa waliosajiliwa kwenye kitabu cha usajili baada ya kufunga biashara ya hisa Jumatano ya tarehe 19 Agosti 2020.

Azimio la kawaida namba 12

“LIAMULIWA KUWA gawio la mwisho la Shi 12.26 kwa kila hisa ya kawaida kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2020 limeidhinishwa.”

6.2 Gawio maalum

Kuidhinisha gawio maalum la Shi 178.57 kwa kila hisa kama ilivyopendekezwa na wakurugenzi. Gawio litalipwa kabla au Ijumaa ya tarehe 13 Novemba 2020 kwa wanahisa waliosajiliwa kwenye kitabu cha usajili baada ya kufunga biashara ya hisa Ijumaa ya tarehe 16 Oktoba 2020.

Azimio la kawaida namba 13

“LIAMULIWA KUWA gawio maalum la Shi 178.57 kwa kila hisa ya kawaida limeidhinishwa.”

7. Ada ya wakurugenzi

Kuidhinisha ada ya wakurugenzi wasio watendaji ya dola za Kimarekani 481 000 kuanzia tarehe 1 Novemba 2020 hadi hitimisho la mkutano mkuu ujao wa mwaka wa Kampuni, ili kuiwezesha Kampuni kuwavutia watu wenye uwezo, ujuzi na uzoefu unaotakiwa ili kutoa mchango unaofaa kwa Kampuni. Hakuna pendekezo la mabadiliko ya ada.

Azimio la kawaida namba 14

“LIAMULIWA KUWA kiwango cha ada ya mwaka ya wakurugenzi wasio watendaji cha dola za Kimarekani 481 000 kimeidhinishwa kwa mchanganuo ufuatao:

| | Pendekelo la ada Dola ya Marekani ¹ | Ada ya sasa Dola ya Marekani |
|---|--|------------------------------------|
| Mwenyekiti wa Bodi | 150 000 | 150 000 |
| Mjumbe wa Bodi | 30 000 | 30 000 |
| Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji | 15 000 | 15 000 |
| Mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji | 8 000 | 8 000 |
| Mwenyekiti wa Kamati ya Ujira | 12 000 | 12 000 |
| Mjumbe wa Kamati ya Ujira | 4 000 | 4 000 |
| Mjumbe wa Kamati ya Uteuzi | 3 000 | 3 000 |

1. Ada hii inajumuisha kodi zote ikijumuisha kodi ya zuio, inayolipwa kwa shilingi ya Kitanzania kwa wakurugenzi wazawa, randi ya Afrika Kusini kwa wakurugenzi wa Afrika Kusini na dola ya Marekani kwa wakurugenzi wengine. Ada hii inalipwa kila robo mwaka (kwa mikupuo minne) kwa mikutano ya kawaida isiyopungua minne kwa mwaka, mikutano maalum mitatu na Mkutano Mkuu wa Mwaka na wa dharura kama itahitajika.

8 Ajenda Maalum

8.1 Uchaguzi wa Mkurugenzi Huru aliyezidi umri wa miaka 70

Kumchagua Jaji (Mstaafu) Thomas B Mihayo kuwa mkurugenzi huru kwa mujibu wa vifungu 194(1) na 194(5) vya Sheria ya Makampuni Sura ya 212 ya mwaka 2002 na kwa mujibu wa kifungu cha 75 cha Katika ya Kampuni.

Azimio maalum namba 1

“LIAMULIWA KUWA, Jaji (Mstaafu) Thomas B Mihayo amechaguliwa kuwa mkurugenzi huru wa Kampuni.”

Ufuatao ni wasifu wa Jaji (Mstaafu) T B Mihayo:

Jaji (Mstaafu) Thomas B Mihayo (74)

Jaji Mihayo ana uzoefu wa zaidi ya miaka 35 akiwa mtumishi wa mahakama mbalimbali Tanzania. Alianza kama Hakimu Mkazi Mfawidhi na akapanda ngazi na kuwa Msajili wa Wilaya hadi kufikia ngazi ya Msajili wa Mahakama Kuu. Aliwahi kuwa Mwanasheria Mkuu wa Shirika la Wanasheria Tanzania; Msajili wa LART – mahakama iliyoanzishwa kwa ajili ya kushughulikia kesi zilizohusiana na madeni ya mashirika ya umma na hatimaye kwa miaka saba kama Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania. Vilevile, Jaji Mihayo aliwahi kuwa mjumbe wa Bodi ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Ununuzi wa Umma; mjumbe wa Bodi ya Benki ya Access na Rais wa Baraza la Habari Tanzania. Pia alikuwa Rais na mjumbe wa Baraza wa Chama cha Wanasheria Tanganyika kwa awamu mbili.

Taarifa ya Mkutano Mkuu *continued*

Hivi sasa, Jaji Mihayo ni Rais wa Chama cha Majaji Wastaafu Tanzania; Kamishna wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Mwenyekiti wa Bodi ya Utalii Tanzania. Pia ni wakili wa Mahakama Kuu ya Tanzania.

Sababu na athari za azimio maalum namba 1

Kukidhi matakwa ya Sheria ya Makampuni Sura ya 212 ya mwaka 2002 ambapo vifungu 194(1) na 194(5) vinahitaji uchaguzi wa mjumbe wa bodi aliye na umri wa zaidi ya miaka 70 kufanyika katika mkutano mkuu baada ya kutoa taarifa maalum kwa wanahisa.

Tarehe ya kufunga rejesta

Tarehe ya kufungwa rejesta ya wanahisa wa Kampuni kwa madhumuni ya kustahili kuhudhuria, kushiriki na kupiga kura kwenye mkutano mkuu wa mwaka ni Ijumaa tarehe 16 Oktoba 2020.

Kushiriki kwa njia ya kielektroniki

Mkutano mkuu wa nne wa wanahisa utafanyika kwa njia ya kielektroniki kama ilivyoainishwa kwenye kifungu 29 na 63 cha Katiba ya Kampuni.

Mkutano mkuu utaoneshwa mubashara kupitia kiunga cha wavuti kwenye simu janja. Wanahisa waliopo kwenye rejesta itakayofungwa tarehe 16 Oktoba 2020 wataweza kujisajili ili kushiriki katika mkutano mkuu. Muongozo wa namna ya kushiriki kwa njia ya kielektroniki pamoja na kujisajili ili kuweza kupata neno la siri utawekwa kwenye tovitu ya Kampuni www.vodacom.co.tz/investors. Kwa taarifa zaidi tafadhali wasiliana nasi kupitia 0800750164.

Wanahisa watawajibika kwa gharama za data na mtandao. Kampuni haitawajibika na upotevu wa mawasiliano kutokana na matatizo ya kimtandao/kuishiwa muda wa hewani/kukatika kwa umeme/na matatizo ya kiufundi ya kielektroniki yanayoweza kuathiri ushiriki wa mwanahisa kwenye mkutano mkuu mwaka kwa njia ya mtandao.

Wanahisa wanahimizwa kutuma maswali yatokanayo na maazimio yaliyopo kwenye taarifa hii kabla ya mkutano mkuu kwenda kwenye barua pepe investorrelations@vodacom.co.tz kabla ya Jumatano ya tarehe 28 Oktoba 2020 saa 4:00 asubuhi. Majibu ya maswali hayo yatatolewa katika mkutano mkuu. Uwasilishaji wa maswali haumzuii mwanahisa kuuliza maswali siku ya mkutano mkuu.

Mahudhurio

Wanaostahili kuhudhuria, kuzungumza na kupiga kura kwenye mkutano mkuu wa mwaka ni wanahisa tu.

Wanahisa wanaweza kuteua wawakilishi kuhudhuria, kutoa maoni na kupiga kura kwa niaba yao. Mwakilishi si lazima awe mwanahisa wa Kampuni. Fomu ya uwakilishi iliyojazwa pamoja na nakala ya hati ya hisa au risiti ya uwekezaji ya DSE ya mwanahisa, kitambulisho cha taifa/kura/leseni ya udereva na taarifa za mawasiliano vitumwe kwa barua pepe kwenda investorrelations@vodacom.co.tz au viwasilishwe kwa Katibu wa Kampuni katika ghorofa ya 7, Vodacom Tower, Ursino Estate, Kiwanja namba 23, Barabara ya Bagamoyo, Dar es Salaam, Tanzania kabla ya saa 4:00 asubuhi Jumatano ya tarehe 28 Oktoba 2020. Fomu ya uwakilishi inapatikana kwenye tovuti ya Kampuni www.vodacom.co.tz/investors.

Upigaji kura utaendeshwa kulingana na Katiba na kanuni za Kampuni. Maazimio ya kawaida yatakayopitishwa katika mkutano mkuu huu yatapaswa kuungwa mkono na zaidi ya 50% ya kura za wanahisa. Azimio maalum litapaswa kuungwa mkono na angalau 75% ya kura za wanahisa.

Wanahisa wenye hisa zisizo kwa majina yao lazima wawapatie watunzaji au wawakilishi wao maelekezo ya kupiga kura katika mkutano mkuu wa mwaka. Kama mtunzaji au mwakilishi wako hatapokea maelekezo kutoka kwako, kama itakavyokuwa, itabidi kufanya maamuzi kulingana na mamlaka uliyoyatoa kwake.

Wanahisa wanahimizwa kutembelea tovuti ya Kampuni kwa taarifa zaidi.

Imeidhinishwa na Bodi



Caroline M Mduma

Katibu wa Kampuni

5 Oktoba 2020

Fomu ya Mwakilishi

Vodacom Tanzania Public Limited Company
(Imesajiliwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)
(Namba ya Usajili 38501)
(ISIN: TZ1996102715 Ticker code: VODA)
("Vodacom" au "Kampuni")

Kifungu A Ijazwe na wanahisa wote

Jina Kamili

Namba ya hati ya hisa (CDS A/c No)

Idadi ya hisa mwanahisa anazomiliki

Kifungu B Ijazwe na wanahisa watakaoteuwa wawakilishi (na si Mwenyekiti) kuhudhuria mkutano kwa niaba yao

Mimi(Sisi), mwenye/wenye hati ya hisa zenye idadi ya hisa za kampuni kwa mujibu wa kifungu A, namteua/tunamteua (angalia maelekezo namba 1&2)

au akishindwa yeye

au akishindwa yeye

Mwenyekiti wa mkutano mkuu wa mwaka kuwa mwakilishi wangu/wetu kuhudhuria, kushiriki mijadala na kupiga kura kwa niaba yangu/yetu katika mkutano mkuu wa mwaka wa nne utakaofanyika kwa nji ya kielektroniki siku ya Ijumaa, tarehe 30 Oktoba 2020 kwa lengo la kutoa maamuzi na kupitisha maazimio ya kawaida na maalum, kupiga kura ya kuafiki au kutokuafiki au kutoshiriki kwenye upigaji kura kulingana na hisa zilizoandikishwa kwa jina langu/letu.

Kifungu C Ijazwe na wanahisa wote

Weka alama x kwenye kisanduku kulingana na matakwa yako.

Vinginevyo mwakilishi wako atapiga kura atakavyoona inafaa.

| | Naafiki | Siafiki | Sishiriki |
|--|---------|---------|-----------|
| 1. Azimio ka kawaida namba 1 Kuthibitisha kumbukumbu za mkutano mkuu wa mwaka uliofanyika tarehe 20 Septemba 2019 | | | |
| 2. Azimio la kawaida namba 2 Kupitisha taarifa za fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2020 | | | |
| 3. Azimio la kawaida namba 3 Kumchagua Nkateko Nyoka kuwa mkurugenzi asiye mtendaji | | | |
| 4. Azimio la kawaida namba 4 Kumchagua Sitholizwe Mdlalose kuwa mkurugenzi asiye mtendaji | | | |
| 5. Azimio la kawaida namba 5 Kumchagua Dejan Kastelic kuwa mkurugenzi asiye mtendaji | | | |
| 6. Azimio la kawaida namba 6 Kumchagua tena Winifred Ouko kuwa mkurugenzi huru | | | |
| 7. Azimio la kawaida namba 7 Kumchagua tena Thembeka Semane kuwa mkurugenzi huru | | | |
| 8. Azimio la kawaida namba 8 Kuchagua Ernst & Young Inc. kuwa wakaguzi wa Kampuni kwa mwaka unaoishia Machi 2021 | | | |
| 9. Azimio la kawaida namba 9 Kumchagua tena Winifred Ouko kuendelea kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji | | | |
| 10. Azimio la kawaida namba 10 Kumchagua tena Thembeka Semane kuendelea kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji | | | |
| 11. Azimio la kawaida namba 11 Kumchagua tena Margaret Ikongo kuendelea kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji | | | |
| 12. Azimio la kawaida namba 12 Kuidhinisha gawio la mwisho la Shi 12.26 kwa kila hisa | | | |
| 13. Azimio la kawaida namba 13 Kuidhinisha gawio maalum la Shi 178.57 kwa kila hisa | | | |
| 14. Azimio la kawaida namba 14 Kuidhinisha ada ya mwaka ya wakurugenzi wasio watendaji ya dola za Kimarekani 481 000 kwa mwaka | | | |
| 15. Azimio maalum namba 1 Kumchagua Jaji (mstaafu) Thomas Mihayo kuwa mkurugenzi huru | | | |

Imetiwa sahihi tarehe

mwezi Oktoba 2020

Sahihi:

Sahihi:

Fomu ya mwakilishi iliyojazwa iwasilishwe kwa Katibu wa Kampuni ya Vodacom Tanzania PLC kabla saa 4 asubuhi, Jumatano tarehe 28 Oktoba 2020.

Maelekezo ya fomu ya mwakilishi

1. Mwanahisa anayepaswa kuhudhuria katika mkutano mkuu anaweza kuteua mwakilishi wake kuhudhuria, kutoa maoni na kupiga kura kwa niaba yake. Mwakilishi sio lazima awe mwanahisa wa kampuni. Kwa makampuni, fomu ya mwakilishi ijazwe na afisa mwenye mamlaka na iwekwe muhuri wa Kampuni husika.
2. Weka alama 'X' kwenye eneo la kujaza kwenye fomu kulingana na kura unayotaka kupiga katika agenda husika. Iwapo utapenda kupiga kura kwa hisa pungufu ya hisa unazomiliki, onyesha idadi ya hisa pungufu ambazo ungependa zipige kura. Iwapo maelekezo haya hayatazingatiwa, mwakilishi atapiga kura atakavyoona inafaa.
3. Mwanahisa anaweza kuweka jina la mwakilishi/wawakilishi wake kwenye sehemu iliyoonyeshwa kwenye hii fomu bila kufuta kipengele cha kuwakilishwa na "Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu wa mwaka" kilichopo chini ya sehemu ya kuandika majina ya wawakilishi. Mwanahisa atapaswa kuweka sahihi yake iwapo atafuta kipengele hicho. Mwakilishi ambaye jina lake limejazwa likiwa la kwanza kwenye fomu ya uwakilishi akihudhuria mkutano mkuu ndiye atahusika kufanya maamuzi.
4. Fomu za mwakilishi zilizojazwa pamoja na hati ya hisa au risiti ya uwekezaji ya DSE ya mwanahisa, ziwasilishwe kwa Katibu wa Kampuni – ghorofa ya 7, Vodacom Tower, Ursino Estate, Kiwanja na 23, Barabara ya Bagamoyo, Dar es Salaam, Tanzania kabla ya saa 4 asubuhi siku ya Jumatano tarehe 28 Oktoba 2020. Aidha, fomu zinaweza kusainiwa kisha kuzituma kwa barua pepe ya investorrelations@vodacom.co.tz.
5. Mwanahisa akifanya masahihisho/mabadiliko yoyote kwenye fomu ya mwakilishi, atapaswa kuwekwa sahihi yake pembeni ya masahihisho/mabadiliko hayo.
6. Wenye hisa wenye umri mdogo kisheria wanapaswa kusimamiwa na wazazi/walezi wao ambao watapaswa kuwa na nyaraka za kisheria za kuwathibitisha.
7. Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu wa mwaka atakubali fomu ya mwakilishi itakavyokuwa imejazwa tofauti na matakwa haya iwapo ataridhika na namna ambavyo mwanahisa atapenda kupiga kura.
8. Kwa wale wenye hisa za pamoja/vikundi:
 - Yeyote kati yao anaweza kutia sahihi kwenye fomu hii
 - Kura ya mwanahisa mkubwa (ukubwa wa hisa utajulikana kulingana na majina yaliorodheshwa kwenye rejista ya wanahisa wa Kampuni) itakayopigwa na yeye binafsi au kutumia mwakilishi, ndio itakayoruhusiwa kwa niaba ya wanahisa wenzake kwenye kikundi.

Ms Caroline Mduma

Katibu wa Kampuni
Ghorofa ya 7, Vodacom Tower, Ursino Estate
Kiwanja na 23, Barabara ya Bagamoyo
P.O. Box 2369
Dar es Salaam
Barua pepe: investorrelations@vodacom.co.tz

Taarifa kuhusu umiliki

| Jumla ya hisa | # ya hisa | % ya hisa |
|---|---------------|-----------|
| Vodacom Group Limited ¹ | 1 680 000 200 | 75.0% |
| Mfuko wa Pensheni wa Wafanyakazi wa Serikali (Uwekezaji wa Shirika la Umma SOC Limited, Jamhuri ya Afrika Kusini) | 164 503 540 | 7.3% |
| Wawekezaji wa Kitaasisi (Afrika Mashariki) | 249 886 242 | 11.2% |
| Wawekezaji wa Kitaasisi (Sehemu nyingine za dunia) | 50 438 753 | 2.3% |
| Wawekezaji wengineo ² | 95 171 565 | 4.2% |
| | 2 240 000 300 | 100.0% |

Note

- Mwaka huu, Vodacom Group Limited ilinunua 26.25% ya hisa zilikuwa zinamilikiwa na kampuni ya Mirambo kama ilivyoainishwa kwenye taarifa ya wakurugenzi
- Jumla ya hisa zinazomilikiwa, ikiwa ni pamoja na hisa zilizo chini ya kiwango cha uchanganuzi. Inaweza kujumuisha umiliki wa hisa za ziada za kitaasisi/rejareja.



Umiliki wa hisa kitaasisi

| | Machi 2020 % Umiliki kitaasisi kwa % |
|---------------------------------|--|
| ● Tanzania | 47.8 |
| ● PIC | 35.4 |
| ● Uganda | 6.0 |
| ● Wanahisa wengine wa kimataifa | 10.9 |
| | 100.0 |

Taarifa za Kampuni

Taarifa za Kampuni

Vodacom Tanzania Public Limited Company

(imeandikishwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)
Usajili namba: 38501
(ISIN: TZ1996102715 Share Code: VODA)

Wakurugenzi

AA Mufuruki¹ (Mwenyekiti), M Ikongo¹ (Mwenyekiti wa Muda), H Hendi⁸ (Mkurugenzi Mtendaji), JJ Marais³ (Mkurugenzi wa Fedha), D Gutierrez⁴, T Streichert⁵, K Gomado⁶, M Mbungela³, ADJ Delpert³, W Ouko², T Semane³, HJC Surtees⁷

1. Mtanzania 2. Mkenya 3. Mwafrika Kusini 4. Mbolivia
5. Mjerumani 6. Mghana 7. Mwingereza 8. Mmisri

Katibu wa Kampuni

Caroline Mduma
15th Floor Vodacom Tower
Plot 23, Ursino Estate
New Bagamoyo Road
P.O. Box 2369
Dar es Salaam, Tanzania

Ofisi iliyosajiliwa

Ghorofa ya 15, Vodacom Tower,
Eneo la Ursino, Kiwanja namba 23, Barabara ya Bagamoyo,
S.L.P. 2369, Dar es Salaam, Tanzania

Mkaguzi wa Hesabu za Fedha

Ernst&Young

Ghorofa ya 4, Tanhouse Tower
Kiwanja namba 34/1, Ursino Kusini Barabara ya Bagamoyo,
S.L.P 2475, Dar es Salaam, Tanzania

Watoa huduma za Kibenki

Citibank Tanzania Limited

Citibank House
Kiwanja namba 1962, Barabara ya Toure, Oysterbay
S.L.P 71625, Dar es Salaam, Tanzania

National Bank of Commerce Limited

Barabara ya Sokoine & Mtaa wa Azikiwe
S.L.P 1863
Dar es Salaam, Tanzania

NMB Bank PLC

Mtaa wa Ohio /Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P 9213
Dar es Salaam, Tanzania

CRDB Bank Plc.

Mtaa wa Azikiwe
SLP 268
Dar es Salaam, Tanzania

Washauri wa Mambo ya Kisheria

Rex Attorneys

344 Barabara ya Toure
Dar es Salaam, Tanzania

IMMMA (Advocates)

Kiwanja namba 357, IMMMA House
Barabara ya Umoja wa Mataifa, Upanga
S.L.P 72484
Dar es salaam, Tanzania

Mtajiri Masuala ya Hisa

CSD & Registry Company Limited (CSDR)

Kambarage House,
Ghorofa ya 2, Mtaa wa 6 Ufukoni
S.L.P. 70081, Dar es Salaam, Tanzania

Mshauri Mkuu aliyesajiliwa wa masuala ya Kumfadhili mjumbe

Orbit Securities Company Limited

Mawasiliano ya Nje
Rosalyann Mworira

Mahusiano na Wawekezaji

Hilda Bujiku, Albert Maneno
investorrelations@vodacom.co.tz
www.vodacom.co.tz/investors

Dai la haki

Taarifa zisizofuata Kanuni za Kimataifa za Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha ('IFRS')

Taarifa hii ina baadhi ya hatua zisizofuata Kanuni za Kimataifa za Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha ambazo hazijapitiwa au kuripotiwa na wakaguzi wa Kundi la Kampuni za Vodacom ('Kundi'). Menejimenti ya Kundi inaamini hatua hizi zinatoa taarifa muhimu za ziada kwa kuelewa ufanisi wa Kundi la Vodacom au biashara za Kundi la Vodacom kwa sababu zinaeleza hatua zilizotumiwa na Kundi la Vodacom kutathimini ufanisi. Hata hivyo, taarifa hizi za ziada zilizowasilishwa hazikufasiliwa kwa njia inayofanana na kampuni zote, ikiwa ni pamoja na zile zilizo katika tasnia ya Kundi la Vodacom. Hivyo, inawezekana haiwezi kulinganishwa na hatua zinazofanana na kutolewa taarifa na kampuni nyingine. Kwa kuongezea, ingawa hatua hizi ni muhimu katika usimamizi wa biashara, hazipaswi kuangaliwa kipwekepeke au kama mbadala, badala yake ziwe kama kijalizo, katika hatua za Kanuni za Kimataifa za Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha. Rejea katika sehemu ya 'Ufanisi wetu' ya taarifa hii kwa maelezo yanayohusiana na mapato ya huduma, EBIT na mapato kwa kila hisa.

Alama za Biashara

Vodafone, logo ya Vodafone, M-Pesa, Vodacom, Wakulima Waliunganishwa na Vodafone Supernet ni alama za biashara za Vodafone Group Plc (au ina program zinazosubiria). M-Fundi, M-Shamba, M-Pawa na Vodacom Faraja ni alama za biashara za Vodacom Tanzania Public Limited Company (au ina program zinazosubiria). Bidhaa zingine na majina ya kampuni yaliyotajwa hapa yanaweza kuwa alama za biashara za wamiliki wao husika.

Matamko ya Matarajio

Taarifa hii, ambayo inajumuisha imeweka matokeo ya awali ya Kundi kwa mwaka unaoishia tarehe 31 Machi 2019, lina 'matamko ya matumaini', ambayo, yanatumika kama yalivyo vingenevyo yameelezwa kwenye Muhtasari uliotolewa na Kampuni tarehe 12 Februari 2017 haujapitiwa au kuripotiwa na wakaguzi wa Kundi, kuhusiana na hali ya kifedha ya Kundi, matokeo ya uendeshaji na biashara na taarifa Fulani zinazohusiana na mipango na malengo ya Kundi la Vodacom. Hasa, matamko hayo ya kuangalia mbele yanajumuisha matamko yanayohusiana na: ufanisi wa baadaye wa Kundi la Vodacom; matumizi ya mtaji siku zijazo, ununuzi, kujitoa, gharama, mapato, masharti ya kifedha, sera ya gawio na maendeleo ya baadaye; mikakati ya biashara na uwekezaji inayohusiana na upanuzi na ukuaji wa Kundi la Vodacom; athari za udhibiti wa biashara za Kundi la Vodacom unaofanywa na serikali katika nchi inapofanya shughuli zake; matarajio ya Kundi la Vodacom kuhusiana na tarehe za uzinduzi na kuanza uuzaji wa bidhaa, huduma au teknolojia; matarajio kuhusu mazingira ya uendeshaji na hali ya soko; ongezeko la wateja na matumizi; na kiwango cha ongezeko la gawio kwa Kundi.

Matamko ya kuangalia mbele wakati mwingine, lakini si wakati wote, hubainishwa kwa matumizi yao ya tarehe katika wakati ujao au Maneno kama 'nita', 'tarajia', 'kusudia', 'ninge', 'weza', 'paswa', 'amini', 'panga' au 'lenga' (pamoja na miundo yao ya ukanushi). Kwa hali yao, matamko ya kuangalia mbele kwa asili yanatabirika, yanaweza kukisiwa na yanajumuisha hatari na mashaka kwa sababu yanahusiana na matumio na yanategemea mazingira ambayo yanaweza kutokea au yasitokee siku za baadaye. Kuna sababu mbalimbali ambazo zinaweza kusababisha matokeo halisi na maendeleo kutofautiana kabisa kuanzia yale yaliyoelezwa au kumaanishwa na matamko haya ya kuangalia mbele. Sababu hizi ni pamoja na, ingawa haziishi hapa, zifuatazo: mabadiliko katika hali ya kiuchumi au kisiasa katika masoko yanayohudumiwa kwa shughuli za Kundi la Vodacom; ushindani mkubwa kuliko ilivyotarajiwa; gharama kubwa kuliko ilivyotarajiwa au matumizi ya mtaji; ongezeko dogo la wateja kuliko ilivyotarajiwa na kupungua kwa wateja wa kudumu; mabadiliko katika hali ya matumizi ya wateja wapya na waliopo; uwezo wa Kundi kupanua nafasi yake kimawanda au kuongeza muda au kuchukua leseni mpya; uwezo wa Kundi kufanikisha kuokoa gharama; uwezo wa Kundi kutekeleza mkakati wake wa kutumia mkongo; kuanza kutoa bidhaa na huduma mpya; huduma za data (mobile data), upanuzi wa Biashara na mtandao wa 4G, mabadiliko katika viwango vya ubadilishaji wa fedha za kigeni, na vilevile katika viwango vya ubadilishaji wa fedha za kigeni, na vilevile viwango vya riba; uwezo wa Kundi kupata faida kutokana na kuingia katika ubia au kufanya biashara pamoja na kuingia katika kufanya biashara ya huduma na utoaji wa leseni ya chapa; matokeo yasiyofaa kwa Kundi ya kufanya na kuchanganya ununuzi na utupaji; mabadiliko katika mfumo wa kisheria ambapo Kundi huendesha shughuli zake; athari za mashauri ya kisheria na mengineyo; kupoteza wasambazaji au kuvurugika kwa mnyororo wa usambazaji; maendeleo katika hali ya fedha ya Kundi, mapato na fedha zinazosambazwa na mambo mengine ambayo Bodi imezingatia wakati wa kuamua viwango vya magawio; uwezo wa Kundi kuwa na mtaji wa kufanyia kazi na mahitaji mengine; mabadiliko katika viwango vya kodi kisheria au mchanganyiko wa faida; na/au mabadiliko katika sharia ya kodi. Matamko mengine yote yaliyofuata ya kuangalia mbele yawe kwa maandishi au mdomo ambayo ni ya Kampuni, kwa mhusika yeyote wa Kundi au kwa watu wowote wanaofanya kwa niaba yao wanastahili katika wingi wao kwa sababu zinarejelewa hapo juu. Uhakika hauwezi kutolewa kuwa matamko ya kuangalia mbele katika waraka huu yatafiikiwa. Kutegemea kufuata sharia na kanuni zinazotumika, Kampuni haikusudii kuboresha matamko haya ya kuangalia mbele na haichukui wajibu wowote wa kufanya hivyo.

